# Nipashe

Jumanne Mei 3, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580934

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



SportPesa

TZS. 1,224,601,040


BET LEO UWE BILIONEA

SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#




**Hospitali** CCBRT yaanzisha kitengo cha uzazi salama

UKURASA 3





Uongozi na wafanyakazi wa Nipashe tunawatakia wasomaji na watangazaji wetu sikukuu njema ya Idd


# 'Panya road' wavamia mtaa wapora, wajeruhi

• **Sita** wakamatwa. Makalla ataja mambo 5 kuwadhibiti... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza baada ya kutoa msaada wa vyakula ikiwamo mchele, mafuta ya kupikia, sukari na mbuzi kwa ajili ya kusherehekea sikukuu ya Eid El Fitr kwa vikundi mbalimbali vya watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## Sheria ya Uhuru wa Vyombo vya Habari kupitiwa

UKURASA 3



## TUCTA: Hatuna shaka na ahadi ya Samia

UKURASA 2


**MICHEZO** MORRISON SAFI KWA NAMUNGO LEO UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira (DAWASA), Mhandisi Cyprian Luhemeja, akiwa ameshika tuzo na fedha taslim Sh. milioni saba alizokabidhiwa na Rais Samia Suluhu Hassan baada ya kuibuka mfanyakazi bora wa Chama cha Wafanyakazi wa Sekta ya Viwanda, Benki na Taasisi za Maji, (FIBUCA), wakati wa kilele cha Siku ya Wafanyakazi mkoani Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Panya road' wavamia mtaa wapora mali

**Na Maulid Mmbaga**

VIJANA wanaodhaniwa kuwa 'panya road' wamedaiwa kuwakata mapanga watu 19 na kupora mali mtaa wa Mtongani Kata ya Kunduchi mkoani Dar es Salaam, huku Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam likithibitisha kuwakamata sita kati yao.

Tukio hilo limetokea siku moja baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuvionya vikundi hivyo kuacha tabia hiyo, wakati akihutubia kwenye maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani, yaliyofanyika mkoani Dodoma, juzi.

Tukio hilo ni la pili katika mkoa huo baada ya wiki moja iliyopita katika Wilaya ya Ilala kundi linalodaiwa kuwa la panya road kuvamia nyumba 23, kujeruhi na kuiba mali na fedha.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, mmoja wa wananchi waliojeruhiwa Kunduchi Mtongani, Tabu Bakari, alisema wakati alipokuwa anarudi nyumbani usiku akiwa na mdogo wake walikutana na kundi la vijana wadogo wengi ambao walimnyang'anya simu yake ya mkononi.

"Tulikuwa tunarudi nyumbani ndipo tukakutana na kundi la vijana wadogo wengi, tulivyokuwa tunazidi kusogea wakasema toeni simu, tulivyotoa wakasema kimbia tulivyofika mbele tukakutana na lingine, wakasema toa simu tukawaambia tumeshatoa, mmoja akanyanyua panga akanipiga nalo kwenye jicho baada ya hapo nilianguka sikuona tena mpaka sasa," alisema Tabu.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amesema katika mkoa wake wanaanzisha operesheni endelevu ya kupambana rasmi na vikundi vya vijana wahuni maarufu panya road.

Makalla, alipokutana na wadau wa ulinzi na usalama jana, alisema hawawezi kuwaacha vijana hao wakitamba na bisibisi na mapanga na kutia hofu kwenye jamii.

"Ni wakati wa kuwaonya panya road kuanzia leo 'jana' baada ya tamko langu usiku wa leo na kuendelea, hakuna panya road atasalimika katika Mkoa wa Dar es Salaam, operesheni inayoanza sio salama kwao na inaenda kuua uti wa mgongo mzima wa mtandao wao katika mkoa huu," alisisitiza Makalla.

"Nitoe onyo baada ya tamko langu wachague kazi nyingine ya kufanya na sio uhalifu katika Mkoa wa Dar es Salaam, niwasihi wazazi kwamba operesheni hii haitawaacha watoto wao wahalifu, kama ataendelea kufanya uhalifu njia sahihi ya kuwapata watoto wenu ni vituo vya polisi vilivyo jirani," alisema Makalla.

Pia alitoa wito kwa wazazi kujua mizunguko ya watoto wao huku akisisitiza hawatakubali kuwa na huruma ya umri wala zana zao kwasababu hao ni wahalifu kama wengine na lengo lao ni kujeruhi na kuua na ameliagiza Jeshi la Polisi kusimama imara.

Alibainisha mambo matano ya kuzingatia wakati wa utekelezaji wa operesheni hiyo ikiwamo, kamati za ulinzi na usalama katika ngazi ya wilaya zinazoongozwa na wakuu wa wilaya kufanya vikao na wenyeviti wote wa serikali za mitaa katika maeneo yao kujadili suala la usalama na namna ya kudhibiti uhalifu katika maeneo yao.

Pili, wakuu wa vituo vya polisi kuongeza doria katika mitaa ya maeneo yao na kuhoji inawezeka vipi watu wateke mitaa mitano na nyumba 23 halafu mkuu wa kituo yupo katika eneo lake.

Makalla alisisitiza maofisa usalama kujipanga na kushirikiana kukomesha uhalifu.

Jambo la tatu, aliagiza wakuu wote wa wilaya kufanya tathmini na kutumia jeshi la akiba la mgambo kusaidia kukomesha tatizo la panya road katika mkoa huo.

Nne, alilitaka Jeshi la Polisi kufanya operesheni ya kuwatafuta na kuwakamata wanunuzi wa mali za wizi kutoka kwa vibaka.

"Taarifa nilizonazo wakati wowote tutazikomboa Tv nyingi kwasababu wanunuzi wameshapatikana na vijana tuliowakamata wanatoa ushirikiano mzuri, kwa hiyo kila unayemkamata akuambie hiyo Tv alitaka kwenda kumuuzia nani, hapa Dar es Salaam kuna watu wanafanyabiashara za bidhaa zinazotoka kwa wahalifu, makamanda mkafanye hiyo kazi bila woga," aliagiza Makalla.

Tano, aliagiza kila wilaya kwa mikoa ya kipolisi kutoa taarifa za kila siku za operesheni ya kuwaondoa panya road, akisisitiza kuwa kila watakapowakamata wawapige picha na kuwatangaza ili familia zao na watu wajue kuwa wako wapi.

Vile vile, alitoa namba ya simu 0787 668 306 ambayo aliwataka wananchi kuitumia endapo wataona dalili ya watu kutaka kufanya uhalifu, huku akisisitiza kuwa operesheni aliyoianzisha haita mwonea mtu badala yake itaenda kudhibiti uhalifu na kuvunja mtandao wa panya road ili mkoa huo ubaki salama.

Aliwahakikishia wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam kuwa hakuna panya road au mhalifu yeyote atakayetamba katika mkoa huo, akiwataka kutulia na kuendelea kusherehekea Sikukuu ya Eid kwa amani kwa kuwa vikosi vya askari vimepangwa kuhakikisha vinaimarisha ulinzi katika mkoa huo.

# TUCTA: Hatuna shaka na ahadi ya Samia

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

SHIRIKISHO la Vyama Huru vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), limesema halina shaka na kauli aliyoitoa Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu nyongeza ya mishahara.

Katika sherehe za Mei Mosi juzi jijini hapo, Rais Samia aliwaambia wafanyakazi kuwa: "Lile jambo letu lipo, si kwa kiwango kilichosemwa na TUCTA kwa sababu mnajua hali ya uchumi wa nchi yetu, hali si nzuri sana uchumi wetu ulishuka chini mno, tumejitahidi sana kwasababu nilishatoa ahadi mwaka jana nimeagiza jambo hili liwepo...Mahesabu yanaendelea tutajua lipo kwa kiasi gani, lakini jambo lipo."

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa TUCTA, Henry Mkunda, alisema: "Sisi tumemshukuru Rais kwa kuonyesha uungwana kwa kuendelea kutimiza ahadi yake hapo awali, tumepokea very positively."

Alibainisha kuwa siku moja kabla ya Mei Mosi 2022, walikutana na Rais, na kwamba walimpelekea hoja 16 ambapo kati ya hizo 13 amezitolea maelekezo ya kufanyia kazi.

"Hili la nyongeza ya mshahara, sisi hatuna shaka na kauli ya Rais kwa kuwa kabla ya sherehe za Mei Mosi tulikuwa naye kwenye kikao cha ndani na alitoa maelekezo kwa Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha kufanyia kazi."

"Suala ambalo lilikuwa ni kiu yetu kubwa ilikuwa ni nyongeza ya mshahara kwa wafanyakazi Mheshimiwa Rais baada ya kukutana naye siku moja kabla ya siku ya Mei mosi tulijadiliana naye kwa undani suala hili na kimsingi alikubali atatuongeza mshahara," alisema.

Alimshukuru Rais kwa kujibu na kukonga nyoyo za wafanyakazi.

"Kwenye hotuba yake amesema tusubiri anakwenda kuyafanyia mahesabu halafu tutapata hiyo mishahara kuanzia mwaka wa fedha unaokuja, ambao unaanza mwezi Julai. Kwa hiyo ni miezi miwili ya kusubiri, tunatarajie haya mambo yanakamilika," alisema.

Alieleza kuwa wafanyakazi ndani ya miezi miwili ijayo kuanzia sasa watarajie ahadi ya Rais aliyoitoa.

"Rais ametuahidi mengine mazuri tu, jambo la watu wa darasa la saba mtakumbuka walivyotolewa kwenye ajira waliachwa tu kama vile wamesahaulika walionekana wamefanya makosa, na wale wenye vyeti feki walionekana wamefanya makosa, lakini safari hii tumeomba serikali na Rais ameahidi walioondolewa kazini kwa kuwa na cheti cha darasa la saba wamerudishwa kazini."

"Pia wale wa vyeti feki waliofanya makosa mama safari hii amekubali kwamba watu hawa ni vizuri wakalipwa, kwanza wakarudishwa nyumbani kwao kwa mujibu wa sheria, lakini michango yao waliyokuwa wakichangia asilimia tano kwenda kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii warudishiwe kwa kipindi chote walichofanya kazi hili ni jambo kubwa," alisema.

# Ufungaji kamera, taa Mirerani waongeza uzalishaji tanzanite

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

KIWANGO cha uzalishaji wa madini ya tanzanite katika eneo tengefu la Mirerani kimeongezeka kutoka kilo 1,968.75 mwaka 2018/19 hadi kilo 3,198.68 kilichozalishwa kuanzia Julai 2021 hadi Machi mwaka huu.

Mafanikio hayo yametokana na kukamilika kwa ujenzi na usimikaji wa miundombinu ikiwamo taa, kamera za ulinzi na barabara inayozunguka ukuta kwa ndani katika eneo hilo.

Waziri wa Madini, Doto Biteko, aliyasema hayo bungeni mwishoni mwa wiki wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2022/23, akieleza udhibiti wa utoroshaji wa madini ya tanzanite katika eneo la Mirerani umeimarika.

Biteko alisema: "Hatua zilizochukuliwa na serikali zimeboresha upatikanaji wa tozo stahiki zinazotokana na biashara ya madini ya tanzanite. Kabla ya ujenzi na usimikaji wa miundombinu, uzalishaji ulikuwa kilogramu 1,964.75 kwa mwaka 2018/2019 ikilinganishwa na kilogramu 3,198.65 za tanzanite zilizozalishwa kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi Machi 2022."

Aidha, Waziri Biteko alisema kazi ya udhibiti wa biashara haramu na utoroshaji wa madini nchini hufanywa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Ofisi ya Usalama wa Taifa, Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji, kamati za ulinzi na usalama za mikoa na wilaya pamoja na raia wema.

Alisema katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, madini ya aina mbalimbali yakiwamo dhahabu, vito, mchanga na madini ya viwandani yenye thamani ya Sh. milioni 501.2 yalikamatwa katika matukio ya utoroshaji na biashara haramu ya madini katika mikoa ya Mbeya, Morogoro, Manyara, Dodoma, Lindi, Geita, Kilimanjaro, Dar es Salaam na Mwanza.

Alisema kutokana na juhudi hizo kumekuwa na ongezeko la ukusanyaji wa maduhuli, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Sh. bilioni 461.6 zimekusanywa na kuwasilishwa katika mfuko mkuu wa Hazina ya serikali, ikilinganishwa na Sh. bilioni 445.2 zillizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2020/2021.

Waziri Biteko alisema mchango wa sekta ya madini kwenye Pato la Taifa umeendelea kuimarika, katika kipindi cha Januari hadi Septemba, 2021 uliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 7.3 kutoka wastani wa asilimia 6.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2020.



# Sheria ya Huduma za Habari kufumuliwa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amesema Bunge linawasubiri kwa hamu wadau wa sekta ya habari nchini, kukamilisha mapitio na maboresho ya Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016 na Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa ya mwaka 2016 na kanuni zake ili kufanya mabadiliko.

Waziri Nape, alitoa kauli hiyo jijini Arusha, wakati akifungua mkutano uliowakutanisha wahariri wa vyombo vya habari nchini na kutoka nje ya Tanzania, wadau wa habari na waandishi wa habari kuelekea kilele cha maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani leo.

"Jukumu letu ni kukamilisha kufanya mapitio ya sheria mbalimbali hasa ile ya huduma ya vyombo vya habari ya mwaka 2016 na kanuni zake za mwaka 2017 na Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa ya mwaka 2016 na kanuni zake.

"Nichukue nafasi hii kumpongeza Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kwa utayari wake, kwa kuwa alinieleza kuwa wanasubiri tukikamilisha mapitio hayo wako tayari mabadiliko katika sekta ya habari iende kwa kasi zaidi.

"Ni matumaini yangu uelewa na uzoefu mtakaoupata katika ushiriki wenu hapa, utasaidia sana katika mchakato wa maboresho na mapitio hayo ili kuwa na sheria bora zinazotunga na Bunge baada ya sisi kukamilisha kazi ya kutoa mapendekezo yetu," alisema.

Katika hatua nyingine, Waziri Nape, alisema kuwa Rais Samia Suluhu Hassan, amethibitisha kuudhuria katika kilele cha maadhimisho hayo na atakuwa mgeni rasmi.

"Ndugu zangu wanahabari mtakumbuka katika historia ya kusherehekea siku ya uhuru wa vyombo vya habari haijawahi kutokea Rais hapa nchini kuhudhuria.

"Rais Samia, ameamua kuvunja rekodi kwa kuhudhuria kwake na huu ni ushahidi kwamba anathamini na kutambua tasinia ya habari na kama mnavyojua itakuwa ni siku ya sikukuu ya Idd el fitr, na kwa hali ya kawaida hata mimi nilipata shaka ya ujio wake, lakini nilipozungumza naye alithibitisha kuwa atakuja.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Jim Yonazi, alisema sekta hiyo inatoa mchango muhimu katika maendeleo ya uchumi wa nchi na dunia kwa ujumla.

Hata hivyo, alisema wizara hiyo, itaangalia fursa zinazotokana na ujio wa ulimwengu wa kidigitali ili kuiwezesha sekta hiyo kuchangia uchumi wa Taifa.

Kadhalika, alisema wizara hiyo, itaendelea kushirikiana na wadau wa habari kuweka mazingira wezeshi kwa kila mmoja kufanya kazi kwa uhuru kwa mujibu wa sheria za nchi.

# CCBRT yaanzisha kitengo uzazi salama

**Na Faustine Feliciane**

KATIKA kuunga mkono juhudi za serikali za kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wakati wa kujifungua, Hospitali ya CCBRT imeanzisha kitengo kipya cha mama na mtoto kuwasaidia wajawazito kujifungua salama huku pia wakiwalenga wanawake wenye ulemavu.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa hospitali hiyo, Brenda Msangi, alisema kitengo hicho kipya kinatarajiwa kufunguliwa rasmi Juni mwaka huu na tayari kimeanza kutoa huduma kwa awamu.

Alisema kinamama wengi wenye ulemavu wanaopata ujauzito wanakuwa na wakati mgumu kipindi cha kujifungua kutokana na huduma zisizo rafiki kwao na kwa kuliona hilo CCBRT itakuwa ikitoa huduma ya kujifungua kwa wajawazito na wasichana wa waliopata mimba wakiwa na umri mdogo.

"Huduma hizi hazitaishia hapo, bali pia kwa wanawake ambao uzazi wao wa kwanza uliwaletea ugonjwa wa fistula, hapa patakuwa sehemu yao ya kujifungulia ili kuepusha tatizo hilo kujitokeza tena," alisema Brenda na kuongeza;

"Kama tunavyojua fistula inatokana na uchungu uliopitiliza kabla ya kujifungua na wengi wanaopata tatizo hili kutokana na huduma duni kwenye baadhi ya vituo vya afya, hapa tutawapa huduma bora na kupambana kuhakikisha tatizo hilo la fistula halijitokezi tena," alisema Brenda.

Alisema hospitali hiyo kwa kushirikiana na Taasisi ya Jakaya Kikwete, Coca Cola na Dar es Salaam Serena Hotel imeandaa hafla ya chakula cha jioni kwa ajili ya kuchangisha fedha zitakazosaidia uendeshaji wa kituo hicho cha Mama na Mtoto, ili kuwasaidia wasiokuwa na uwezo gharama.

"Hafla hii itafanyika Mei 7, Serena Hotel na lengo letu ni kukusanya Dola za Kimarekani milioni mbili (zaidi ya Sh. bilioni tano) ambazo zitasaidia uendeshaji wa kitengo ikiwa ni pamoja na rasilimali watu na vifaa, tunaomba wadau wengine wajitokeze kusaidia juhudi za kuwakomboa wajawazito, mabinti wanaoshika mimba wakiwa na umri mdogo pamoja na wanawake wenye ulemavu pindi wanaposhika mimba," alisema Brenda.

Pia alisema tayari wameandaa namba maalum ya kuchangia fedha kiasi chochote kwa Watanzania na wadau namba hiyo ni 200500 kwa mitandao yote ya simu.

Kuhusu gharama za matibabu kwenye kitengo hicho, alisema wapo ambao watachangia matibabu kutokana na uwezo wao na ambao hawatalipia gharama baada ya kufanyiwa tathmini na kitengo cha ustawi wa jamii kujua uwezo wao.

Kwa upande wake mwakilishi wa Kampuni ya Coca Cola, Victor Amos, alisema kampuni hiyo imeguswa na juhudi za CCBRT kuisaidia serikali kutoa huduma bora na kupunguza vifo vya kinamama na watoto wakati wa kujifungua na wameona ni vyema kujitokeza na kushirikiana nao.

Mmoja wa kinamama mwenye ulemavu aliyejifungua hivi karibuni hospitalini hapo, Zabibu Almasi, alisema huduma bora za kitengo hicho kipya cha CCBRT kimemsaidia kujifungua salama watoto mapacha.

"Huu ni uzazi wangu wa pili, uzazi wa kwanza nilijifungia hospitali nyingine, lakini huduma zake hazikuwa rafiki, hata miundombinu yake ilikuwa kikwazo sana kwangu kutokana na ulemavu, nashukuru kitengo hiki kipya kina huduma zote ambazo mlemavu anatakiwa kupata wakati wa kujifungua hata baada ya kujifungua, nashukuru nimejifungua mapacha wakike na wakiume, watoto wangu wana afya na hata mimi nipo na afya nzuri," alisema Zabibu.

Alisema kuwa hajatumia gharama zozote kwa kuwa alipata mfadhili aliyemsaidia kulipia.

Naye Magdalena Joseph, aliyejifungua hospitalini hapo, alisema uzazi wake uliotangulia mtoto alizaliwa na tatizo na wakati alipopata ujauzito wa pili alikutana na daktari anayefanya kazi hospitalini hapo ambaye alimshauri kupata huduma kwenye kitengo hicho.

"Nashukuru mtoto wangu huyu nimejifungua salama na ana afya nzuri, hii yote ni kutokana na huduma nzuri na ya karibu niliyoipata hapa, kwa kweli nashukuru sana," alisema Magdalena.


DRC DANISH REFUGEE COUNCIL

## TANGAZO LA ZABUNI

SHIRIKA LA DANISH REFUGEE COUNCIL LINATARAJIA KUINGIA MKATABA WA UNUNUZI WA VIFAA VYA KUTENGENEZEA MKAA MBADALA.

SHIRIKA LA DANISH REFUGEE COUNCIL LILILOPO KIBONDO LINAWAARIKA WAZABUNI KULETA BEI ZAO.

NYARAKA ZA KUJAZIA BEI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISH REFUGEE COUNCIL KIBONDO KUANZIA TAREHE 2.05.2022 HADI TAREHE 16.05.2022 SIKU ZA KAZI SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30 JIONI. TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO.

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA +255624 399 911 au BARUA PEPE josphat.mwangi@drc.ngo

ZABUNI ZITAFUNGULIWA TAREHE 18.05.2022 SAA 4:00 ASUBUHI OFISI ZA DANISH REFUGEE COUNCIL KIBONDO NA KAMATI YA KUFUNGUA ZABUNI LA DANISH RFUGEE COUNCIL PEKEE KUTOKANA NA MLIPUKO WA UGONJWA WA UVIKO-19. HIVYO WAWAKILISHI WA KAMPUNI HAWATORUHUSIWA KUSHIRIKI UFUNGUZI.

UNAWEZA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA RFQ.TZA@drc.ngo AU KULETA MOJAKWA MOJA OFISINI VINGINEVYO NI BATILI.

216835502



Wateja wakinunua kuku katika Soko la Manzese jana kwa ajili ya Sikukuu ya Idd inayofanyika leo duniani kote jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Hoja za CAG mikopo HESLB zafanyiwa kazi

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

SERIKALI imeanza kufanyia kazi hoja za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) zilizoibuliwa kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Mwaka 2020/21, ambapo imeunda timu ya kukagua mifumo ya utoaji mikopo itakayofanya kazi ndani ya miezi miwili.

Katika hoja za ukaguzi za CAG, ilionyesha kuna wanafunzi wengine wamepata mikopo na wengine kunyimwa licha ya kuwa na vigezo vya kupata.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa kwenye ziara ya kukagua ujenzi wa Chuo cha Ufundi Dodoma, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema amekutana na Bodi ya HESLB na kuzungumza nao na wameanza kufanyia kazi hoja hizo za CAG kabla ya kwenda bungeni.

"Tumepata maelezo ambayo tutayafanyia ukaguzi vizuri zaidi kwamba kwa mfano wewe ni yatima unastahili kupata mkopo unapopeleka zile taarifa upeleke zikiwa zimekamilika, usipopeleka zikiwa zimekamilika wakati wa kuchakata unaweza kukosa mkopo wakati unastahili kupata," alisema.

Alibainisha kuwa kutokana na hilo, imeundwa timu ya watu watatu ambao ni kutoka Tanzania Bara na Zanzibar ambayo itapitia mifumo na kuangalia namna inavyopata taarifa zilizoingizwa na wanafunzi.

"Timu hii itafanya kazi itatoa taarifa kwangu na kwenye Bodi ya Mikopo ili kuangalia nini cha kuboresha zaidi, nichukue fursa hii kutoa wito kwa wale wote wanaoomba mikopo waweke taarifa zote zinazohitajika, usije ukakosa kuweka taarifa ikaonekana taarifa yako haijakamilika, halafu kumbe unastahili kupata mkopo ukaukosa," alisema.

Alisema timu bado haijaanza kufanya kazi anatarajia kukutana na kiongozi wa timu kesho mkoani Morogoro na baadaye kukutana na wajumbe wote na bodi hiyo ili kupewa hadidu za rejea.

"Timu hii ina wataalamu wabobezi wa mifumo ambao wanaweza kutumia programu yeyote, na 'team leader' ni mtaalamu wa hesabu ili kwenda kuangalia mifumo inavyofanya kazi, kwasababu hakuna mfumo uliokamilika duniani hata siku moja, pia itaangalia kinachowezekana na tutatoa muda wa kumaliza kazi tusingependa ipite miezi miwili kabla ya kupewa taarifa kwa kuwa hao ni wataalamu wazuri wa mifumo,"alisema.

**UPATIKANAJI VITABU**

Kuhusu hoja ya CAG ambayo alibaini vitabu vya kiada milioni moja kati ya milioni sita ndivyo vilivyopelekwa kwenye shule nchini, Prof. Mkenda alisema "Kwenye ripoti ya CAG kuna mambo mengi lakini tutayajibu bungeni nitazungumzia mambo mawili kwanza kwenye vitabu hivi karibuni nilileta wadau wote wa vitabu pamoja na taasisi yetu ya elimu kuzungumza kwanza changamoto iliyokuwapo ya kiasi kuna wengine walisema wanapata shida kupata vitabu katika Taasisi ya Elimu."Alieleza kuwa baada ya mkutano huo iliundwa kamati ya wadau ambayo imeundwa na Kamishna wa Elimu ili kufuatilia upatikanaji wa vitabu, tayari imeanza kazi na italeta taarifa Julai mwaka huu kwenye mkutano wa wadau.

Prof. Mkenda alisema dhamira ya serikali ni kupunguza gharama za uchapishaji wa vitabu na kuweka ushindani kwa kuwawezesha Watanzania wenye uwezo wa kuchapisha vitabu wafanye hivyo ili kuongeza upatikanaji wake nchini.

"Kulikuwa na ucheleweshaji kidogo wa vitabu vya darasa la saba ambao ulitokana na logistics nimeambiwa vimefika na vimepelekwa, lengo letu huko mbele ni kuwa na vitabu vya kutosha kabisa katika shule tunataka gharama za uchapishaji vitabu zipungue," alisema.

Alieleza kuwa wanataka waangalie namna ya kutumia Teknolojia ya Habari (TEHAMA) kwa kuhakikisha vitabu vinapatikana mtandaoni na kuimarisha maktaba nchini.

**RASIMU YA MITAALA**

Katika hatua nyingine, Waziri Mkenda alisema chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan yatafanyika mageuzi makubwa ya elimu ambayo hayajawahi kutokea tangu Tanzania ipate uhuru ambapo rasimu ya mitaala mipya itatoka Desemba mwaka huu.

"Kazi kubwa ya mitaala imefanyika na tumekusanya maoni zaidi ya 100,000, lakini ukikutana na mtu anakuuliza mnafanya nini kwenye elimu, sasa kutakuwa na makala kwenye televisheni,"alisema.

Alibainisha kutakuwa na kongamano kubwa la elimu mwishoni mwa mwezi Mei mwaka huu na litafanyika kwa siku tatu ambalo watapata maoni zaidi na watakutana na wabunge Mei 7, mwaka huu, ili kuwaeleza hatua zilizofikiwa kwenye kukusanya maoni ya mitaala na kupokea maoni yao.

"Mwaka huu kazi ya kukusanya maoni na kuchakata ikamilike, mwishoni mwa Desemba tumalize tuwe na rasimu inayoingia kwenye maamuzi serikalini na ikiingia utekelezaji uanze mapema kabla ya mwaka 2025, tulitarajia kuanza mwaka 2026 lakini naamini kwa jinsi tulivyojipanga utekelezaji utaanza 2024 angalau kwa awamu," alisema.

## Ushirikiano ZTC, NMB wamvutia Rais Mwinyi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), imeeleza kuvutiwa na ushirikiano kati ya Kamisheni ya Utalii Zanzibar (ZTC) na Benki ya NMB ambao umekuwa chachu ya kukuza utalii.

Kadhalika, imetaka kuziunga mkono wizara zote za SMZ na Mamlaka za Serikali za Mitaa, ili kuziwezesha kuziona fursa na kuzitumia kwa ustawi wa Uchumi wa Zanzibar.

Hayo yamesemwa na Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban, alipokuwa akiwasilisha salamu za Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, katika hafla ya futari iliyoandaliwa na NMB, ikihudhuriwa na mawaziri wa SMZ, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, viongozi wa dini na wateja wa benki walioko visiwani hapo.

Akizungumza wakati wa kutoa neno la shukrani mbele ya waalikwa zaidi ya 400, Waziri Omar, ambaye alimwakilisha Rais Mwinyi, alisema ushirikiano wa NMB na ZTC ni mkubwa, ulioifungamanisha kamisheni hiyo na fursa za kiuchumi, na kwamba Rais anatamani kuona NMB inazifikia wizara mbalimbali na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

"Niko hapa kwa niaba ya Rais, Dk. Hussein Mwinyi na nichukue nafasi hii kuwapa salamu zake. Kwanza Rais amefarijika sana kwa aina ya ushirikiano uliokuwapo baina ya NMB na Kamisheni ya Utalii Zanzibar, ushirikiano ambao unalenga zaidi kukuza utalii wa Zanzibar. Ushirikiano huo unaangalia mbali zaidi ya yale tuliyoyazoea.

"Kwa muda mrefu utalii wetu ulikuwa umejikita katika kuuza fukwe, lakini NMB mmenyoosha mkono kwa ZTC na kuwaonyesha fursa zingine za kiutalii zilizoko Zanzibar, hasa vivutio vya historia na mambo kale. Ni jambo zuri, la kupongezwa na kuungwa mkono.

"Pia, SMZ inawakaribisha zaidi NMB kushirikiana na wizara yenyewe ya utalii kwa ujumla wake, najua ina mipango mingi mbali ya ile ya Kamisheni, lakini pia mshirikiane na wizara zingine zote za SMZ, kuanzia Wizara ya Elimu, Wizara ya Fedha, Wizara ya Kilimo, hata Wizara ya Biashara na Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa.

"Mkikaa na Mstahiki Meya atawaambia fursa zilizoko katika kuendeleza miji na majiji yetu. Kwa hiyo niwaalike NMB mshirikiane na wizara zingine na naamini mtashiriki kwa mapana katika kuendelea kuuimarisha uchumi wa Zanzibar, kupitia dhana hii inayochakatwa na Rais Dk. Mwinyi ya Uchumi wa Buluu," alisisitiza Waziri Omar.

Aidha, alibainisha kuwa yeye binafsi amefarijika sana kusikia NMB inaiunga mkono SMZ sio tu katika masuala ya utalii, bali uwekezaji wao wenye thamani ya Sh. bilioni 1 za kujenga Kituo cha Pamoja cha Malipo (One Stop Center), bandarini, ambacho kitakuwa chachu ya ufanisi na kukuza makusanyo.

Ofisa Mkuu wa Wateja Wakubwa na Serikali wa Benki ya NMB, Alfred Shao, alisema NMB imekuwa na mahusiano ya muda mrefu na ZTC, ambako mashirikiano yao hayajaishia tu katika kuimarisha Sekta ya Utalii kwenye fukwe za bahari, bali pia unaangazia utamaduni wa Mzanzibar na vyakula asilia.

"Hafla hii inafanyika katika muktadha huo wa mashirikiano baina yetu. Tunafanya mambo mengi katika Sekta ya Utalii, lengo ni kuunga mkono jitihada za Serikali ya Zanzibar, kwani tunatambua Sekta ya Utalii ni kati ya maeneo yanayoingizia pesa nyingi sana serikali, nasi tumeelekeza nguvu zetu huko," alisema Shao.

HABARI KITAIFA

# Mfumo uagizaji pamoja mafuta ulivyoepusha bei kupaa zaidi

Na Jenifer Gilla

LICHA ya taifa kupitia changamoto ya ongezeko la bei ya mafuta ya petroli na dizeli inayotokana na ongezeko la bei ya nishati hiyo kwenye soko la dunia, imebainishwa kwamba huenda changamoto hiyo ingekuwa kubwa zaidi iwapo taifa lisingekuwa linatumia mfumo wa uagizaji wa pamoja wa nishati hiyo.

Kwa mujibu wa Kamishna wa Petroli na Gesi Wizara ya Nishati, Michael Mjinja, uwapo wa mfumo wa uagizaji wa nishati ya mafuta kwa pamoja unaotekelezwa kupitia Wakala wa Ununuzi wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) umeliokoa taifa kutoingia kwenye changamoto ya ukosefu wa nishati hiyo kabisa kama ilivyotokea kwa baadhi ya mataifa jirani.



"Bei za mafuta bado zinapanda na huenda utulivu usiwepo hivi karibuni lakini jambo la uhakika hapa kwetu upatikanaji ni wa uhakika, mafuta yaliyoko yanatosha na yataendelea kuwapo kadri ilivyopangwa," alisema.

"Uhakika huu tunaupata kwa kuwa mfumo tunaoutumia kuingiza nishati hii kwa kuwa unatuwezesha kuwa na mipango thabiti na uhakiki wa taarifa zote muhimu kuhusu hali ilivyo," alisema Mjinja alipohojiwa na kituo kimoja cha televisheni nchini mwishoni mwa wiki.

Alisema kabla ya kuanzishwa kwa mfumo wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja, Tanzania nayo ilikuwa ikikumbana na changamoto za kukosekana kwa mafuta kwa kuwa mfumo uliokuwapo ulitoa fursa kwa wafanyabiashara kuagiza nishati mmoja mmoja kwa wakati anaoona unafaa kulingana na mahitaji yake.

"Gharama za kuleta mafuta zilikuwa juu sana, shehena ilikuwa inaletwa na meli ndogo ndogo, hivyo zilikuwa zinajazana bandarini na zilikuwa zinatumia muda mwingi kushusha hadi siku 40, jambo ambalo lilikuwa halitoi uhakika wa upatikanaji wa nishati hiyo," alisema Mjinja.

Alisema utaratibu huo ulikuwa hautoi uhakika wa utulivu wa bei kwani serikali ilikuwa haina uwezo wa kufuatilia na kujua bei halisi ya mafuta na gharama za usafirishaji, lakini hakukuwa na uwezo wa kuhakikisha upatikanaji wa nishati hiyo unaenda sambamba na mahitaji.

Kwa mujibu wa Mjinja, ni kutokana na sababu hiyo ndipo serikali iliona umuhimu wa kuanzisha utaratibu wa ununuzi wa pamoja ili kumlinda mwananchi na athari za bei isiyoendana na uhalisia pamoja na kulihakikishia taifa upatikanaji wa uhakika wa nishati hiyo muhimu.

"Kwa sasa kampuni za uuzaji wa mafuta ya jumla zipo 39 kila mmoja anawasilisha mahitaji yake kisha mafuta yanaagizwa kwa pamoja, miezi miwili kabla ili kuhakikisha hakuna upungufu. Hii inatusaidia serikali kujua mahitaji na kiasi tulichonacho," aliongeza Mjinja.

Akihojiwa kupitia kipindi hicho cha televisheni, Meneja wa Biashara ya Petroli wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA), Kemilembe Kafanabo, alisema kuwa zabuni za kuingiza mafuta hayo nchini zimekuwa zikitangazwa kwa uwazi ili kuruhusu kampuni zenye uwezo na vigezo vya kuingiza nishati hiyo kwa bei shindani aweze kushiriki.

"Kwa hiyo kama kuna mwagizaji anajua namna anavyoweza kupata nishati hii kwa bei nafuu zaidi fursa ndio hiyo kushiriki katika zabuni hizi. Kuna kampuni 23 ambazo ndizo hushiriki zabuni hizi na kwakuwa washiriki wa zabuni hizi ni wengi pia inakuwa sio rahisi kwao hata kupanga njama ya kibiashara ya kupandisha bei ya mafuta," alisema Kafanabo.

Kwa mujibu wa Kafanabo, pamoja na mambo mengine, majukumu ya PBPA ni pamoja na kukusanya mahitaji na kuratibu uagizaji wa nishati hiyo kabla ya mahitaji hayo kupelekwa EWURA kwa ajili ya uhakiki ili kuona kama yanaendana na uhalisia kabla ya kuruhusu mchakato kuendelea.

Kauli hizo zinaungwa mkono na mtaalamu wa uchumi na mtafiti mwandamizi, Dk. Hoseana Lunogelo, aliyesema mfumo wa ununuaji mafuta kwa pamoja una manufaa makubwa kwa walaji wa mwisho (wananchi) kuliko changamoto zake.

Kwa mujibu wa Dk. Lunogelo, utaratibu wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja unapunguza gharama kwa kuwa anayepewa zabuni ya kuleta mafuta ni yule anayetoa gharama ya chini, lakini gharama za meli zinakuwa chini kwa kuwa mzigo unaletwa kwa wingi kwa wakati mmoja huku pia kukiwa hakuna gharama ya usubirishaji wa meli.







TANZANIA PORTLAND CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY

twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

## TAARIFA KWA WANAHISA

Taarifa inatolewa kwa wanahisa wote wa Tanzania Portland Cement Public Limited Company kwamba Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa utafanyika:

**Ramada Beach Resort, Grand Ocean Hall, Ground Floor**
**Jangwani Beach, Plot 170-171,**
**Mbezi Beach, Dar es Salaam,**
**siku ya Jumatano, tarehe 25 Mei 2022, saa nne asubuhi.**

**DONDOO**

1. Ufunguzi wa Mkutano: Katibu kusoma taarifa iliyotolewa kuuita Mkutano Mkuu na kuhakiki kama akidi ya Mkutano imetimia.
2. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 29 uliofanyika tarehe 25 Mei 2021.
3. Kupokea, kujadili na kama zitaafikiwa kupitisha taarifa ya wakurugenzi, taarifa ya wakaguzi na taarifa ya fedha kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Desemba 2021.
4. Kupokea, kujadili na kama litaafikiwa kuthibitisha gawio la mwaka 2021.
5. Kuthibitisha uteuzi wa wakaguzi wa mahesabu kwa mwaka unaoisha tarehe 31 Desemba 2022.
6. Kuthibitisha kuchaguliwa upya kwa wakurugenzi Bi Ruth Zaipuna na Bw Oswald Urassa watakaowakilisha wanahisa wenye hisa chache kwenye Bodi ya Wakurugenzi hadi mkutano mkuu wa mwaka 2025.
7. Azimio Maalum: Kujadili na kama itaafikiwa, kupitisha maboresho na mabadiliko kwenye Katiba ya Kampuni (Memorandum and Articles of Association) ya kampuni, kama yalivopendekezwa na Bodi ya Wakurugenzi, yanayolenga kukidhi matakwa ya Soko la Hisa la Dar es Salaam.
8. Kujadili mambo mengine ya kampuni ambayo taarifa zake zimepokelewa.

**Kwa Niaba ya Bodi**
**Tarehe: 2 Mei, 2022**

**Katibu wa Kampuni**

1. Mwanahisa yeyote aliye na haki ya kuhudhuria na kupiga kura kwenye mkutano, anaruhusiwa kuteua mwakilishi au wawakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake. Fomu ya kuteua mwakilishi inapatikana kwenye tovuti ya kampuni **(https://www.twigacement.com).**
2. Mwakilishi atakayeteuliwa siyo lazima awe mwanahisa wa kampuni. Fomu ya kuteua mwakilishi ambayo imejazwa na mwanahisa inatakiwa iwasilishwe kwenye ofisi za kampuni, Wazo Hill, Dar es Salaam angalau masaa 24 kabla ya muda wa kuanza mkutano, la sivyo fomu itakuwa haijakidhi vigezo.
3. Kwa ajili ya utambulisho, mwanahisa anatakiwa kuja na cheti cha umiliki wa hisa pamoja na kitambulisho chake (pasi ya kusafiria, leseni ya udereva, au kitambulisho cha taifa, cha kazi, au cha mpiga kura).
4. Mahesabu kamili ya kampuni, ambayo yamepitishwa na wakaguzi, yanapatikana kwenye ofisi za kampuni, Wazo Hill, Dar es Salaam, au pia kupitia tovuti ya kampuni **(https://www.twigacement.com).**

HEIDELBERGCEMENT

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunasherehekea uhuru wa habari, lakini bado changamoto hazijaisha

**LEO** ni maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani, kwa Afrika yanafanyika Tanzania kwa kuwaleta pamoja wanahabari na wadau wa habari wa nchi mbalimbali chini ya kauli mbiu ya 'uandishi wa habari na changamoto za kidigitali'.

Kila mwaka maadhimisho haya yanafanyika kutathmini hali ya utendaji wa vyombo vya habari na wanahabari wenyewe, ili kuhakikisha mazingira mazuri ya utendaji kazi utakaowezesha upatikanaji wa taarifa.

Tanzania tunasherehekea tukiwa na matokeo chanya kwenye taaluma, kwamba serikali imeonyesha utayari wa kushirikiana na wadau kufanya mabadiliko ya sheria za habari ambazo zinakwaza utendaji kazi.

Lakini kumekuwa na utayari wa serikali kusikiliza wadau na wanahabari hali iliyoongoza kujitathmini kulikokuwa kumeshamiri kiasi cha maudhui nzuri kukosekana kwa hofu ya kuwakwaza watawala au kuchukuliwa hatua.

Tunaamini mchakato huu utashirikisha wadau wote wa habari kutoa maoni yao ili yanapofanyika marekebisho yabebe mahitaji ya wanataaluma wote, badala ya kundi moja au wachache kupewa kipaumbele.

Jana Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema serikali iko tayari kushirikiana na wadau wote wakati wowote na mchakato wa mabadiliko utakuwa shirikishi huku akiwahakikishia Rais Samia Suluhu Hassan anawapenda wanahabari na ndiyo maana amesukuma kuwapo mabadiliko.

Moja ya mambo yaliyoibuka wakati wa kongamano la wanahabari kuelekea siku ya leo ni ukuaji wa teknolojia na namna vyombo vya habari vya magazeti, redio na TV vinavyoweza kuendana na mabadiliko hayo kwa kuziona fursa zilizoko kujipati mapato.

Pia, umuhimu wa umoja kwa wanahabari na taasisi zao barani Afrika, kwa kuwa changamoto zinafanana kama mabadiliko ya sheria kandamizi yanasambaa kutoka nchi moja kwenda nyingine, kuzimwa au kupunguzwa nguvu kwa intaneti hasa wakati wa uchaguzi mkuu.

Yote hayo yanakwaza uhuru wa kujieleza na upatikanaji wa taarifa; kwamba mabadiliko hayo na watawala kutaka kunyamazisha vyombo vya habari Afrika, ni suala lenye kututaka tuwe wamoja wenye sauti moja linapotokea jambo ambalo siyo la maendeleo ya uandishi wa habari.

Jingine ni ukuaji wa teknolojia uliotoa nafasi kwa raia kutumia intaneti kusambaza taarifa mbalimbali ambazo siyo za kitaaluma, kisha kujiita wanahabari na inapokuwa haina maadili jamii inawalaumu wanahabari kuwa wakosaji walioshindwa kufanya kazi yao kwa mujibu wa maadili.

Pia, waandishi wa habari bado wana hali duni za maisha kwa sababu baadhi ya vyombo vya habari haviwalipi au vinachelewesha malipo yao kwa muda mrefu kiasi cha wengi kugeuka ombaomba, jambo linalohitaji mikakati ya pamoja kutatua vinginevyo maadili yataendelea kuwa kitendawili.

Aidha, ukuaji wa vyombo vya habari mtandaoni ambavyo maudhui yake haikidhi matakwa ya uandishi wa habari, hali inayoifanya taaluma kudharaulika na kuonekana kila mtu anaweza kuifanya.

Kongamano hilo linatuleta pamoja kuziona changamoto na tunaposherehekea siku hii muhimu, lazima kushirikiana na wadau wote ikiwamo serikali, ili inapofanya mabadililo ya sheria nasi wanahabari tubadilike kwa ambayo yapo ndani ya uwezo wetu katika kutatua.

Lazima tuendelee kuelimisha jamii na kutengeneza tofauti ya waandishi wa habari waliosomea na wanaotambulika kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Habari 2016, na wananchi wanaorusha taarifa kwenye mitandao yao ya kijamii.

Tunapoadhimisha siku hii tunapaswa kuona umuhimu wa kuendelea kupaza sauti juu ya umuhimu wa haki ya taarifa ambayo wananchi wanastahili kupata habari hasa kwa serikali ambayo inawajibika kwao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wanahabari watumie uhuru huu kikamilifu

**LEO** ni kilele cha maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani, ambayo huadhimishwa Mei 3 ya kila mwaka kwa lengo la kukuza uelewa wa umuhimu wa uhuru wa tasnia ya habari.

Aidha, yanakumbusha kuviheshimu pia ili kulinda haki ya kupata habari kwa kila mmoja kwa kuwa ni taarifa sahihi ndizo zinazoleta uelewa na kujua mambo.

Uhuru wa vyombo vya habari na wanahabari ni moja ya haki ya msingi ya kiraia inayoipa jamii haki ya kupata habari na kusambaza taarifa, haki ya uhuru wa kujieleza na haki ya uhuru wa maoni ambazo ni nguzo muhimu katika kuzingatia misingi ya demokrasia.

Ni kwa mantiki hiyo, Rais Samia Suluhu Hassan, amewahi kugusia uhuru huo na kuagiza kufunguliwa kwa vyombo vya habari vilivyofungiwa huku akiwataka wahusika kutotumia ubabe kuvidhibiti.

Pamoja na hayo, akashauri vyombo vya habari visifungiwe kibabe akisema; "Watakapofanya makosa adhabu zitolewe kulingana na sheria inavyoelekeza, viacheni vifanye kazi yao isionekane wanazuiwa kuongea."

Kauli kama hiyo kutoka kwa kiongozi wa nchi, inatia matumaini kwamba anatambua na kuthamini mchango wa vyombo vya habari kwa jamii na taifa kwa kuwa bila hivyo hakuna kuenea taarifa kutoka kwa wananchi kwenda kwa viongozi na kwa wanaowaongoza kwenda kwa umma, na anaagiza viheshimiwe.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye naye anaongeza kuwa anataka vyombo vya habari visisite kuikosoa serikali, huku akitaka ukosoaji uwe wa kujenga na siyo kubomoa, kwa kuwa vikiikosoa serikali bila kutoa mbadala ikakasirika itakuwa siyo vizuri.

Kwa kauli hizo, ni wazi kuna dhamira ya dhati ya kudumisha uhuru wa vyombo vya habari, hivyo ninadhani sasa ni wajibu wa waandishi wa habari kutumia uhuru huo vizuri, kwani hakuna uhuru usio na mipaka.

Ni wazi kwamba serikali inatambua umuhimu wa vyombo vya habari kufanya kazi kwa uhuru na kujali uzalendo wa nchi bila kuvunja sheria, hivyo suala la kutambua mipaka ya uhuru wanaopewa ni la muhimu.

Wajibu wa waandishi wa habari ni kuwa mastari wa mbele kuhabarisha umma wa Watanzania kwa kutoa taarifa kwa kuzingatia maadili yanayoongoza tasnia ya habari na kufuata sheria na katiba ya nchi.

Iwapo waandishi watakwenda kinyume wanaweza kujikandamiza wenyewe kwa vyombo wanavyofanyia kazi kufungiwa, kutokana na kukiuka maadili na kubaki wakilalamika kukandamizwa, kumbe makosa yanaweza kutoka kwao.

Miaka ya hivi karibuni, vyombo vya habari vimeendelea kuongezeka nchini vikiwamo vya mitandao ya kijamii, hali inayoonyesha uwapo wa uhuru wa vyombo hivyo, jambo la msingi ni kufanya kazi kwa kuzingatia maadili.

Ninaamini kwamba Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani ni nafasi ya pekee ya kuwapa waandishi fursa ya kutafakari na kuenzi wajibu wao muhimu kwenye jamii kama kioo kinachoimulika.

Hivyo ingependekeza kama kila mmoja atahakikisha anatimiza wajibu wake inavyotakiwa, katika kuendeleza taaluma hiyo ambayo ina umuhimu mkubwa kwenye jamii na taifa linalotegemea pia tasnia hiyo kwa maendeleo.

Iwapo kila mwandishi atazingatia maadili ya kazi yake, hakutakuwa na ongezeko la usambazaji wa taarifa zisizo sahihi na za uzushi kupitia mitandao yaa kijamii ambazo zimekuwa zikijitokeza kila mara.

Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani isaidie kuwabadilisha wale ambao wamekuwa wakijisahau na kujikuta wakisambaza taarifa zisizo sahihi na kusababisha taharuki kwenye jamii, badala yake wafuate maadili.

HABARI KITAIFA

## Shirika lawapatia wakazi Moro hati za kimila 403

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Kilimo Endelevu Tanzania (SAT) kwa kushirikiana na Serikali ya Wilaya ya Mvomero wamefanikisha kutoa hati za kimila 403 kwa wakulima na wafugaji, wakazi wa vijiji vya Lubungo na Mbingo.

Hati hizo ni miongoni mwa utekelezaji wa mradi wa kukuza ushirikiano baina ya wakulima na wafugaji ili kupunguza migogoro kati yao.

Akizungumza wakati wa ugawaji wa hati hizo Meneja mradi wa kukuza ushirikiano baina ya wakulima na wafugaji, Rashid Mallya, alisema mchakato wa utoaji hati hizo ulianza miezi 10 iliyopita.

"Wakati tunaendelea kutekeleza mradi wa mashirikiano ambao tulianza tangu mwaka 2017, tulibaini kuwa miongoni mwa changamoto ni wanakijiji kutokuwa na hati za mashamba au viwanja ndiyo maana mtu alikuwa anaweza kuingia hadi katika eneo la mwenzake," alisema.

Alisema kupatikana kwa hati hizo kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa mogogoro ya wakulima na wafugaji kwasababu kila mmoja atakuwa na umiliki wa eneo lake na kutambua mipaka iliyoko baina ya shamba moja na lingine.

Pia, hati hizo zitatoa fursa ya wafugaji kumiliki maeneo yao na kuyaendeleza katika kilimo cha malisho mifugo bila kuingia katika mashamba ya wakulima.

Akikabidhi hati hizo kwa wananchi hao, Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Halima Okash, alilipongeza Shirika la SAT kwa kuwezesha upatikanaji wa hati hizo kwa lengo la kupnguza migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo imekuwa ikijitokeza mara kwa mara.

Alisema serikali itaendelea kuunga mkono jitihada zinazofanywa na wadau kuwaletea wananchi maendeleo.

"Ni wapongeze kwa kutimiza jambo hili ni kubwa sana na serikali tutaendelea kuwaunga mkono, lakini niwaombe wananchi wenzangu wa Mvomero tukazitumie vizuri hizi hati hasa ziwasaidie kiuchumi na kijamii, kusiwepo na migogoro tena wilayani kwetu," alisema.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mbingo, Rashid Kibukila, alisema wamefarijika kupata hati hizo ambazo kwa kiasi kikubwa zitawasaidia katika masuala mbalimbali ikiwamo upataji wa mikopo kwa ajii ya kijikwamua kiuchumi.

Alisema mara nyingi taasisi za kifedha zinahitaji mali isiyohamishika ili kutoa mikopo. "Tunashukuru kwasababu licha ya kutusaidia kutatua migogoro ya ardhi, lakini muhimu zaidi itatusaidia kijamii na kiuchumi hasa kwenye mikopo na hata kuwawekea dhamana ndugu zetu wapokabiliwa na kesi mahakamani," alisema.

Naye Shehekangai Agilo, mfugaji mkazi wa kijiji cha Lubungo, alisema baada ya kupata hati hizo watatumia elimu waliyoipata kuendelea maeneo yao ambayo sasa wanayamiliki kisheria.

# Makamba awaondoa hofu wazalishaji nguzo umeme

**Na Francis Godwin,** IRINGA

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amesema nguzo zote za ujenzi wa miradi ya umeme nchini zitanunuliwa Tanzania na hakuna mkataba wowote uliosainiwa wa kuagizwa nje.

"Naomba kuwatoa hofu wenye viwanda vya nguzo za umeme nchini kuwa nguzo zote zitakazotumika kujenga miradi ya umeme zitatoka hapa hapa nchini tunachoomba ni ubora wa nguzo zetu na nimeteua kamati ya watu 12 itakayofanya kazi ya kujua ubora wa nguzo zetu na zile za nje ili tuzalishe nguzo bora zinazokubalika ndani na nje ya nchi," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, aliwapongeza wabunge wa Mkoa wa Iringa kwa umoja katika kutetea ajenda za kimaendeleo zinazohusu mkoa wao.

Waziri Makamba alitoa kauli hiyo jana mjini Mafinga, wilayani Mufindi wakati wa kikao cha pamoja na wadau wa mazao ya misitu kutoka Njombe na Iringa.

Alisema shabaha ya serikali ni kuendelea kuunga mkono jitihada za viwanda vya nguzo vya ndani ili miradi yote ya umeme kuendelea kutumia nguzo zinazochakatwa na viwanda vya ndani.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umeme nchini, Maharage Chande, alisema agizo la waziri halina mjadala na sasa kinachofuata ni utekelezaji wa agizo hilo na miradi yote ya usambazaji umeme nchini itatekelezwa kwa nguzo za ndani.

Kwa upande wake Sendiga, alipongeza umoja wa wabunge wa Mkoa wa Iringa kwa kupigania ajenda za mkoa wao hasa suala la nguzo za umeme kuendelea kununuliwa nchini kuwa ni jambo la kizalendo kwa kuwa linaenda kuongeza mapato kwa serikali na wananchi.

Sendiga alisema, mikoa ya Iringa na Njombe ndiyo iliyouza nguzo zaidi ya asilimia 90 zilizotumika kusambaza umeme nchini na walishangazwa kusikia hoja ya kuwa nguzo za ndani sio bora wakati nyingi zimesimikwa vijijini na ni imara.

"Tukushukuru mheshimiwa Waziri wa Nishati kwa kufika leo na kufanya maamuzi haya ambayo yana afya kubwa kwa uchumi wa mikoa hii miwili na taifa," alisema.

Mbunge wa Jimbo la Kilolo, Justin Nyamoga, aliipongeza Wizara ya Nishati chini ya Waziri Makamba kwa kuwa sikivu.

Alisema ameona dhamira ya dhati ya Wizara ya Nishati kushughulikia na kumaliza kero kubwa ya ununuzi nguzo za ndani na kama msimamo wa serikali ungekuwa wa kununua nguzo nje ya nchi, madhara yake yalikuwa makubwa kwa uchumi wa Halmashauri za mikoa ya Iringa na Njombe.

Mbunge wa Jimbo la Makete, Festo Sanga aliipongeza serikali kushughulikia malalamiko ya wadau wa uchakataji nguzo za umeme nchini na kuwa kilio chao hakikuwa cha wakazi wa Njombe na Iringa pekee, bali cha taifa.

Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga, alimpongeza Waziri Makamba kutatua kero ya ununuzi wa nguzo za ndani.



Baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa katika Kata ya Mzinga, jijini Dar es Salaam wakiwa katika mafunzo ya kujengewa uwezo wa kuripoti vitendo vya rushwa ya ngono na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na wasichana wenye nia ya kuwania nafasi mbalimbali za uongozi kupitia vyama vya siasa, yaliyotolewa na kituo cha taarifa na maarifa Kipunguni mwishoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Chuo cha Ufundi Dodoma kuanza mwakani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema Chuo cha Ufundi Dodoma, (DTC) kinachotarajia kuanza kutoa elimu ya ufundi mwakani na kuagiza watendaji wa wizara hiyo kuanza kutafuta wakufunzi, vifaa na vitendea kazi.

Chuo hicho kwa awamu ya kwanza kitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,500 na kutoa fani tatu za kipaumbele nchini ambazo ni nishati, vifaa tiba na ujenzi.

Akizungumza jana baada ya kukagua ujenzi wa chuo hicho eneo la Lugala unaofanywa na mkandarasi kutoka kampuni CRJE, Prof. Mkenda alisema awamu hiyo itakamilika Desemba mwaka huu na utagharimu Sh. bilioni 17.9.

"Ni chuo kikubwa na kitakuwa chuo cha nne nchini na kitachukua wanafunzi wengi na kitakapokamilika kabisa kina uwezo wa kuchukua wanafunzi 3,000 lakini kwa awamu hii ya ujenzi inayofanyika itachukua wanafunzi 1,500, awamu ya kwanza inatumia Sh. bilioni 17.9," alisema.

Waziri huyo alisema kutakuwa na ubadilishanaji wa wakufunzi kutoka nje ya nchi kwenye chuo hicho ili kutoa elimu bora ya ufundi na ujuzi katika chuo hicho.

"Tuna vyuo kama hivi vya ufundi kimoja ni DIT ambacho kina kampasi Mwanza pia, Mbeya na Arusha, hivyo kikikamilika hiki tutakuwa na vyuo vinne ambavyo vitatusaidia kuandaa wanafunzi fani ya ufundi...Tutakuwa na exchange staffs tuchukue wataalamu wa nje wakae hapa nchi kama Uturuki tunataka tuchukue wafundishe kwa mwaka mmoja hapa na sisi twende kule," alisema.

Alisema vyuo vya Mamlaka ya Ufundi Stadi (VETA) vinavyofanya kazi vipo 43 lakini serikali inatarajia mwisho wa mwaka huu kuwa na vyuo 77 vinavyofanya kazi baada ya ujenzi wa majengo yake kukamilika.

"Tuna vyuo 25 vya wilaya vinajengwa, vinne vya mikoani, ukichukua hivi 43 na vingine tutafikia 77, kazi kubwa ni kuhakikisha vifaa vinawekwa na kuwa na wakufunzi wa kutosha kwenye vyuo hivyo,"alisema.

Alisema vyuo vya ufundi vya serikali na binafsi vilivyoko nchini ni 831.

Alisema ujenzi huo utakapokamilika mwishoni mwa mwaka huu atamwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuweka jiwe la msingi.

"Umeme, maji na barabara vinahitajika kwenye eneo hili... Ujenzi wa awamu ya pili tunatarajia uanze mwaka 2023 na jumla ya ujenzi wote unatakiwa kutumia Sh. bilioni 100 kuna ujenzi mkubwa zaidi umebaki huko mbele," alisema. Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Ufundi wa Wizara hiyo, Dk. Noel Mbonde, alisema ujenzi wa vyuo vya ufundi utaongeza vijana wenye ujuzi kwa zaidi ya asilimia 30.

"Kwa mwaka kwenye mafunzo ya ufundi tunapata wahitimu wasiopungua 150,000, kwa elimu ya ufundi wa kati kwa mwaka tunapata kwa wastani 150,000," alisema.

Meneja wa mradi huo, Gao Yuqi, alisema Watanzania 260 kwa wiki wanafanya kazi kwenye mradi huo huku akihakikishia serikali kuwa watakamilisha ujenzi kwa wakati kwa mujibu wa mkataba wao ili ifikie malengo yake ya kutoa elimu ya ufundi.

# Waadhimisha Siku ya Wafanyakazi kwa kutembelea kaburi la Magufuli

**Na Daniel Limbe,** CHATO

KATIKA kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani kundi la watumishi 40 wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Sumve, iliyoko wilayani Kwimba mkoani Mwanza, wametembelea kaburi la hayati Dk. John Magufuli.

Hatua hiyo imelenga kutambua mchango wake kwa wafanyakazi nchini, jitihada na maono yake kwa wafanyakazi hayatosahaulika daima.

Akizungumza na Nipashe, Mkuu wa shule hiyo, Xaveria Thomas, alisema kutokana na mafanikio ya kimaendeleo yaliyopatikana enzi za utawala wa hayati Dk. Magufuli, wamelazimika kutumia Siku ya Wafanyakazi Duniani kutembelea kaburi lake nyumbani kwake katika kijiji cha Rubambangwe, Mlimani wilayani Chato, mkoani Geita.

"Hayati Dk. Magufuli, alikuwa mfanyakazi aliyependa na kuithamini sana kazi yake... kwa hiyo kutembelea kaburi lake na kufanya ibada fupi ya maombezi kwetu wafanyakazi wa shule ya sekondari ya wasichana Sumve tunaona fahari sana," alisema.

Mwalimu Raulian Milengo, aliiomba serikali kuendeleza ndoto za hayati Dk. Magufuli kwa kusisitiza watu kufanya kazi kwa bidii badala ya kutegemea misaada kutoka nje ya nchi.

"Ni vyema serikali yetu ikayaendeleza mazuri yote yaliyoasisiwa na hayati Dk. Magufuli ikiwa ni pamoja na kukamilisha miradi iliyoachwa pamoja na kuwataka wananchi kufanya kazi kwa bidii...kwa kuwa ndiyo kipimo cha utu na mafanikio katika maendeleo," alisema Milengo.

Kwa upande wake, mwalimu Jovinus Bwire, alisema, kupitia siku hiyo wafanyakazi anajifunza uthubutu, uadilifu, upendo na imani kwa hayati Dk. Magufuli kwa kuwa enzi za uhai wake amewahi kuwa mwalimu wa Shule ya Sekondari Sengerema iliyoko mkoani Mwanza.

"Kwa hiyo sisi walimu tunajivunia kazi yetu kupitia hayati Dk. Magufuli kwa kuwa ni moja ya walimu waliokuwa na maono makubwa kwa maendeleo ya jamii...ndiyo maana tunajivunia kutoka Mwanza hadi Chato mkoani Geita," alisema Bwire.



Rais wa Chama cha Wakunga Tanzania (TAMA), Feddy Mwanga, akizungumza katika warsha ya waandishi habari jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, ambayo iliandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Masuala ya Afya ya Uzazi na Idadi ya Watu (UNFPA), Tanzania, kwa lengo kutaka watambue majukumu ya ukunga. **PICHA: SABATO KASIKA**

# UNFPA: Tutashirikiana na serikali kuwapatia huduma bora wajawazito

**Na Yasmine Protace**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Masuala ya Afya ya Uzazi na Idadi ya Watu (UNFPA), Tanzania, limeahidi kushirikiana na serikali ili kuhakikisha huduma bora za wanajawazito zinaendelea kupatikana nchini.

Ahadi hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Naibu Mwakilishi Mkazi wa shirika hilo, Dk. Wilfred Ochan, katika warsha ya waandishi wa habari iliyolenga kuwajengea uelewa kuhusu majukumu ya wakunga.

"Changamoto mpya kwa sasa katika nchi nyingi duniani ni uhaba wa wakunga na inafanyiwa kazi ili kuondokana na vifo vingi vitokanavyo na uzazi ifikapo 2030, tunatarajia kuyafikia malengo endelevu ya kupunguza vifo chini ya asilimia 70 kati ya vizazi hai 100,000," alisema Dk. Ochan.

Alisema, UNFPA inaendelea kushirikiana na Wizara ya Afya na Chama cha Wakunga Tanzania (TAMA) ili kuhakikisha inawajengea uwezo wa kitaaluma wakunga katika maeneo mbalimbali nchini.

"UNFPA pia imeboresha huduma za afya zikiwamo ukarabati wa wodi za wazazi kwenye baadhi ya mikoa ikiwamo ya Kigoma, Dodoma, Simiyu na Zanzibar," alisema.

Ofisa Programu wa Afya ya Mama na Mtoto wa shirika hilo, Furaha Mafuru, alisema, wakunga wakiwezeshwa watasaidia kuokoa maisha ya mama mjamzito na mtoto.

"Vifo vya kinamama ni changamoto na wakunga wanatakiwa kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi, hivyo wakiwezeshwa kwa kupewa vitendea kazi wanaweza kufanya kazi yao kwa ufanisi," alisema Mafuru.

Alifafanua kuwa ifikapo mwaka 2030 upungufu wa wakunga duniani unaweza kufikia 700,000 na kwamba inatakiwa kila nchi kuhakikisha wanaongezeka ili kupunguza vifo vya wajawazito na watoto.

Rais wa Chama cha Wakunga Tanzania (TAMA), Feddy Mwanga, alisema kuna sababu mbalimbali zinazochangia vifo vya mama wajawazito ikiwamo kifafa cha mimba, upungufu wa damu na maambukizi ya VVU.

"Lakini vifo hivyo vinaweza kutoka kama kama kutakuwa hakuna mkunga katika kituo cha afya, hivyo ni muhimu kuwapo kwa wakungwa wa kutosha ili kusaidia kuokoa maisha ya mama na mtoto," alisema Mwanga.

Siku ya Wakunga Duniani inatarajiwa kufikia kilele chake Mei 5 mwaka huu ambapo maadhimisho kitaifa yatafanyika jijini Dodoma.

## Wajawazito washauriwa kuhudhuria kliniki mapema

**Na Julieth Mkireri,** KIBITI

KIONGOZI wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Sahil Geraruma, amesema ili kufanikisha kuondoa tatizo la udumavu kwa watoto ni lazima wajawazito waanze mapema kuhudhuria kliniki kwa ajili ya kupata ushauri wa kitaalamu.

Alisema tatizo la udumavu linaanza kujitengeneza kuanzia mama akiwa mjamzito endapo hatazingatia mlo kamili na ushauri wa wataalamu kuhusiana na vyakula.

Geraruma aliyasema hayo jana wilayani Kibiti wakati wa kuzindua na kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo iliyotekelezwa katika wilaya hiyo.

"Mbio za Mwenge wa Uhuru zinazidi kutukumbusha kuhusiana na lishe bora serikali inawasisitiza wajawazito kuhudhuria kituo cha afya mapema kupata ushauri wa kitaalamu ikiwamo vyakula vinavyotakiwa," alisema.

Alisema watoto wakiwa na udumavu hawawezi kufanya vizuri darasani na itasaidia kuwaandaa vijana walioelimika na watakaotengeneza uchumi wao na wa taifa kwa ujumla.

Geraruma pia aliwakumbusha wazazi kuzingatia malezi ya kimaadili kwa watoto wao na kufuatilia tabia kuwaepusha kujiingiza kwenye makundi ya uhalifu.

Alisema kitendo cha kutozingatia malezi bora inasababisha baadhi ya vijana kujiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya ambayo yanakatisha ndoto za vijana na kuleta athari kijamii na kitaifa.

Alitoa maelekezo kwa watendaji kufuatilia miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwenye maeneo yao ili ikamilike kwa muda uliopangwa na iendane na thamani ya fedha zilizotolewa.

"Zingatieni pia kutunza nyaraka za manunuzi kwenye miradi ili kuepusha sintofahamu ambayo inaweza kutokea ukaguzi unapofanyika," alisisitiza.

Awali, akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka Wilaya ya Fufiji, Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Kanali Ahmed Abas, alisema Mwenge huo utakimbizwa katika miradi 15 ya wilaya hiyo yenye kata tano ambayo ina thamani ya zaidi ya Sh. 869,550,520.

Moja ya miradi iliyozinduliwa ni wa kisima cha maji katika zahanati ya kikosi cha Jeshi 830 kilichogharimu Sh. milioni 20 chenye uwezo wa kuzalisha lita 11,300 kwa saa.

Taarifa ya mradi huo ilieleza kuwa kikosi hicho kimetoa zaidi ya Sh. milioni 15 kupima wingi na ubora wa maji pamoja na kujenga mnara na kukunua tangi la kuhifadhia maji na utawanufaisha maofisa wa kikosi hicho pamoja na wananchi wanaopata huduma katika zahanati hiyo.

# Ndalichako ataka mazingira ya usalama na afya kazini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, amewataka waajiri na wafanyazi kushirikiana kujenga utamaduni bora wa kuweka mazingira yenye usalama na afya ili kuzuia vihatarishi katika maeneo ya kazi.

Prof. Ndalichako ameyazungumza hayo mwishoni mwa wiki katika maadhimisho ya Siku ya Usalama na Afya Mahali Pa Kazi Duniani yaliyofanyika kitaifa Jakaya Kikwete Convention Centre, jijini Dodoma.

Alisema waajiri na wamiliki wa sehemu za kazi katika maeneo mengi hudhani kuweka mazingira ya kazi salama ni gharama za ziada kutokana na ukosefu wa ufahamu wa faida za kuboresha mazingira ya kazi ili waweze kutambua hasara zinazoweza kutokea hususan inapotokea ajali au ugonjwa katika sehemu ya kazi.

"Kwa ujumla ukiwauliza wafanyakazi sababu ya ajali kutokea, wengi wao watajibu ajali ni matokeo ya mazingira mabaya ya kazi na ukiwauliza waajiri wao watajibu kuwa ajali husababishwa na uzembe wa wafanyakazi.

Hivyo, tunapoadhimisha siku hii leo, ni vema kuwahimiza wadau wote wawe na mjadala mpana wa namna ya kuimarisha utamaduni wa kuzuia vihatarishi miongoni mwa jamii yetu," alisema Prof. Ndalichako.

Akitoa taarifa ya maadhimisho ya mwaka huu Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema lengo la maadhimisho hayo ni kuendeleza kampeni za kuhamasisha uwepo wa mazingira salama na yenye kulinda afya za watu katika sehemu za kazi.

Alieleza kuwa kampeni ya mwaka huu imejikita zaidi katika kuhakikisha kuwa kunakuwa na ushirikishwaji katika ngazi zote za maamuzi wakiwamo wafanyakazi ili nao wawe sehemu ya maamuzi na hivyo kujenga utamaduni wa kukinga zaidi kuliko kusubiri mambo yaharibike ndipo hatua za kuyarekebisha zichukuliwe.

"Utamaduni huu ukijengeka utapelekea kupunguza ajali, magonjwa na vifo vinavyotokana na mazingira hatarishi ya kazi na hivyo kuongeza tija katika uzalishaji ndani ya Taifa letu," alisema Khadija.

Alizitaja shughuli zinazotekelezwa katika kampeni ya uhamasishaji ya mwaka huu ni pamoja na; Mafunzo ya Usalama na Afya kwa wajasiriamali wadogo katika sekta mbalimbali wakiwamo wachimbaji wadogo, wazalishaji wa mazao ya misitu, wenye viwanda vidogo chini ya SIDO, watu wenye ulemavu pamoja na wanafunzi wa vyuo vya ufundi stadi na elimu ya juu.

Shughuli nyingine ni maonyesho ya usalama na afya mahali pa kazi, shindano la tuzo za usalama na afya mahali pa kazi miongoni mwa maeneo mbali mbali ya kazi pamoja na ukaguzi wa mifumo ya usalama na afya katika ofisi za wizara na ofisi mbalimbali za serikali.

# Shilingi milioni 400 kufungua miundombinu barabara mpya

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

HALMASHAURI ya Manispaa ya Morogoro inatarajia kutumia Sh. milioni 400 kwenye ya bajeti ya mwaka wa fedha wa 2022/2023 kwa ajili ya kufungua miundombinu ya barabara mpya katika maeneo ya kata za pembezoni na kuzikabidhi kwa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) ili kuingizwa katika mipango ya kuzihudumia.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Ally Machela, alisema hayo wakati akijibu swali la papo kwa papo kutoka kwa Diwani wa Kata ya Kihonda, Hamis Kilongo, kwenye kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani la Manispaa ya Morogoro.

Alitaka kujua mkakati wa sasa kwa manispaa hiyo ili kuhakikisha barabara zilizoko kwenye mitaa ya kata zote 29 ambazo kwa sasa hazipitiki kutokana na kutokarabatiwa kwa muda mrefu kupitia wakala uliopewa dhamana na serikali. Akijibu swali hilo, alisema katika kuendelea kuboresha miundombinu ya barabara zilizoko kwenye mitaa ya kata hizo, halmashauri ya manispaa hiyo itaendelea kushirikiana na TARURA kwa ajili ya kupanga na kuweka msukumo zaidi ili barabara ziweze kufanyiwa maboresho.

"Kutokana na uzito wa jambo hili linalojitokeza kila mwaka, Manispaa kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 imetenga Sh. milioni 400 zitakazotumika kufungua barabara mpya na baadaye kuzikabidhi TARURA ziweze kuingizwa kwenye mipango yao ili zihudumiwe," alisema Machela.

Kwa upande wake Meya wa Manispaa hiyo, Pascal Kihanga, alisema ili kuondokana na changamoto hiyo ni vyema kwa sasa halmashauri zikanzaa kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa katapila litakalotumika kuchonga barabara zilizopo kwenye mitaa ya kata zake 29 ili kuboresha huduma za kijamii na kiuchumi.

"Kama sisi manispaa tukiwa na katapila letu kutarahisisha kuboresha miundombinu ya barabara zetu na hilo litafanyika kwa kushirikiana na wezetu wa TARURA ambao bado kwa sasa hawazifikii barabara zote kulingana na bajeti zao," alisema Meya Kihanga.



Mbunge wa Jimbo la Ushetu (CCM) mkoani Shinyanga, Emmanuel Cherehani, akizungumza na wananchi wa Kata ya Bukomela katika ghala la kuhifadhi tumbaku, wakati wa ziara yake ya kusikiliza kero mbalimbali zinazowakabili wananchi katika sekta ya elimu, afya, maji na miundombinu ya barabara jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Washerehekea Siku ya Dunia kwa kupanda miti

**Na Jenifer Gilla**

KATIKA kusherehekea Siku ya Dunia, wadau wa mazingira nchini wamepanda miti katika Shule ya Msingi Lioness Migulani, wilayani Temeke, jijini Dr es Salaam ikiwa ni kuunga mkono juhudi za serikali ya kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi wa Taasisi ya Tanzania Cleanup and Conservation Initiative (TCCI), Salum Kigungo, alisema kuwa wameitumia siku hiyo kupanda miti ili kuwaandalia vizazi vijavyo urithi wa mazingira mazuri na salama.

"Tunaposema kuwekeza tunamaanisha kuwatengenezea mazingira mazuri vizazi vyetu vijavyo kwa kuwa tusipowekeza leo basi huko mbele hali itakuwa mbaya.

Kwa hiyo tumeamua huu utakuwa ndio utaratibu wetu, leo tumeanzia hapa na siku nyingine tunakwenda kwingine hadi tunakapojiridhisha na hali ya uwepo wa miti nchini," alisema Salum.

Naye Sarah Pima, alisema wameamua kupanda miti katika shule hiyo ili kuwafundisha wanafunzi hao jinsi na umuhimu wa kupanda miti ili nao waje kuwa walimu wazuri na waendeleze utamaduni huo kwa vizazi vijavyo.

"Kama kaulimbiu ya mwaka huu katika siku ya dunia inavyosema 'wekeza katika sayari yetu' basi tumewekeza katika kutoa elimu ya upandaji miti ambayo itawasaidia leo na vizazi na vizazi. Kwa hiyo leo tumewekeza kwa kupanda miti ya matunda, maua na vivuli," alisema Sara.

Mtaalamu wa mabadiliko ya tabianchi, Nyendo Kinyonga, alisema wana jukumu la kuilinda dunia dhidi ya majanga yatokanayo na utunzaji wa mazingira ikiwamo athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kuwa binadamu ndiyo wahusika wakubwa wa uharibifu wa mazingira hayo.

"Changamoto mojawapo ya athari za mabadiliko ya tabianchi ni kutotabirika kwa majira na tunaona jinsi inavyotuathiri nchini. Sasa hivi wakulima wanalalamika mvua za masika hazikunyesha kwa wakati, hali inayosababisha wengine wasilime kwa hiyo hali ikiendelea hivi inaweza kusababisha njaa," alisema.

Kwa upande wake, mwanachama wa Lions Club of Dar es Salaam, Janki Sinha, alisema wameguswa kushiriki upandaji wa miti katika shule hiyo kutokana na kutambua kwa sasa nchi na dunia inahitaji miti ya kutosha ili kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Shirika letu linatoa huduma za kibinadamu katika maeneo matano ambayo ni mazingira, kisukari, macho, chakula na saratani, tumeguswa kushiriki katika upandaji miti kuunga mkono juhudi za serikali katika kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi," alisema.

Naye Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira katika Halmashauri ya Wilaya ya Temeke, Ally Khatib, alisema kuwa halmashauri inatambua mchango wa wadau wa mazingira nchini na kusihi kuwa serikali itaendelea kuunga mkono jitihada hizo ili kuweka mazingira ya nchi katika hali ya kuvutia na kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Miti hii ninayopandwa leo haina budi kutunzwa ili ije kuleta manufaa kwa vizazi vijavyo. Tukienda na utaratibu huu tutakuwa tunapanda miti mwaka mzima, lakini faida zake sizionekane na hakutokuwa na maana ya shughuli hii tuliyoifanya leo," alisema Khatibu.

Mkuu wa Shule ya Msingi Lioness Mibulani, Hadija Mzuzuri, aliwashukuru wadau hao kwa kuchagua shule yao kupanda miti kwa kuwa kutaboresha mazingira ya shule hiyo na kutengeneza mazingira rafiki kwa wanafunzi hao kufurahia masomo yao.

Aliwaomba wadau hao kumsaidia kutatua changamoto wanazokumbana nazo ikiwamo uhaba wa matundu ya vyoo ambayo ina matundu sita ya vyoo kwa wavulana 602, huku wasichana 569 wakitumia matundu matano pekee.

Naye mwanafunzi wa darasa la sita katika shule hiyo. Nizar Burham aliwashukuru wadau hao kwa kuwapandia miti shuleni hapo kwa kuwa itasaidia kuleta hewa safi na mazingira kuwa katika hali nzuri.




Meneja wa Usalama, Afya na Mazingira wa Kampuni ya Tigo, Nashon Mdalla, akipokea tuzo ya usalama na afya mahala pa kazi kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, katika maadhimisho ya Siku ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi, iliyoandaliwa na OSHA, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtoto afariki Pemba kwa kutumbukia kwenye shimo

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MTOTO wa kike mwenye umri wa miaka mitatu (3) amefariki dunia baada ya kutumbukia kwenye shimo la maji machafu Mjini Wingwi, Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, Juma Sadi Khamis, alimtaja marehemu huyo kuwa ni Riziki Ali Faki ambaye alitumbukia kwenye shimo la maji machafu lililokuwa nje ya nyumba yao.

Alisema kuwa, tukio hilo lilitokea Aprili 20 mwaka huu, majira ya saa 12:00 jioni huko Mjini Wingwi Micheweni. Baada ya Jeshi la Polisi kupokea taarifa hiyo, lilifika katika eneo la tukio na kumchukua mtoto huyo kumpeleka katika Hospitali ya Micheweni kwa ajili ya uchunguzi, ambapo aligundulika tayari ameshafariki.

"Baada ya Jeshi la Polisi kupata taarifa hii, tulifika na kumpeleka mtoto hospitali, ambapo daktari alithibitisha kwamba amefariki kutokana na kunywa maji mengi," alisema kamanda huyo.

Aliitaka jamii kufukia mashimo yote yaliyoko karibu na nyumba zao, ili kuepusha madhara mbalimbali yanayoweza kujitokeza, ikiwamo vifo.

"Hiki ni kipindi cha mvua, hivyo tuhakikishe yale madimbwi na mashimo yote tuyafukie kwani yanahatarisha usalama wa watoto," alieleza.

Aidha, aliwataka wazazi na walezi kuwa karibu na watoto wao katika kipindi chote, ili kuepusha majanga yanayoweza kuepukika.

## Wenye ualbino watakiwa hadhari kukwepa ukatili

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha Watu wenye Ualbino Tanzania (TAS) kimewaomba watu wenye ulemavu huo na familia zao kuchukua kila aina ya tahadhari ili kuhakikisha wanaepuka vitendo vya ukatili dhidi yao.

Wito huo ulitolewa jijini Dar es Salaam juzi, na Katibu wa TAS, Mussa Kabimba, alipozungumza na waandishi wa habari kuelezea masikitiko ya chama hicho kufuatia kuwapo kwa taarifa za kunusurika kuuawa kijana mwenye ualbino.

"Nitoe rai kwa watu wenye ualbino na familia zao kuendelea kuchukua tahadhari kwa ajili ya usalama wao wakati wote ikiwamo kutoa taarifa polisi, kwenye vyombo vyenye mamlaka vilivyo karibu yao wanapoona viashiria vya uhalifu ili vidhibitiwe haraka ikiwamo kuwakamata mapema wanaojihusisha na vitendo hivyo," alisema Kabimba.

Alisema, chama hicho kimepokea kwa masikitiko taarifa za kutaka kukatwa mkono kijana mwenye ualbino ambaye ni mkazi wa Mabibo Dar es Salaam, ambapo mbali na kuwataka watu wenye ulemavu kuchukua tahadhari, aliliomba Jeshi la Polisi kuwasaka na kuwakamata watuhumiwa.

Katibu huyo aliongeza kuwa tukio hilo limejitokeza miezi michache tangu kufukuliwa kaburi la mwanaume mwenye ualbino aliyetajwa kwa jina la Heri Shekighenda lililotokea Novemba mwaka jana mkoani Tanga.

"Pia tunaiomba wizara husika na vitengo vyake vinavyosimamia ustawi wa watu wenye ulemavu nchini, zifanyike kampeni za uelimishaji jamii kuhusu ualbino na kukemea imani potofu zinazochangia mauaji ya albino," alisema.

Alisema, kwenye suala la utoaji wa elimu, aliomba vyombo vya habari, viongozi wa dini, asasi za kiraia pamoja na viongozi wengine wa serikali kushiriki katika kuelimisha umma ili kuhakikisha albino wanakuwa salama.

"Pamoja na hayo tunaomba kukamilishwa kwa mchakato wa kupitisha rasimu ya mpango mkakati wa kitaifa wa watu wenye ualbino (2022-2026) iliyokabidhiwa Ofisi ya Waziri Mkuu Februari mwaka huu," alisema.

# Wazazi, walezi wachangishana kujenga matundu ya vyoo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BAADHI ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Ngokolo Kata ya Bukomela katika Halmashauri ya Ushetu wilayani hapo, wanalazimika kujisaidia vichakani na milimani kutokana na upungufu wa matundu ya vyoo.

Shule hiyo ina wanafunzi 857 kati yao wa kike 441 na wa kiume 416.

Kwa sasa shule ina matundu nane ya vyoo ambayo hayatoshelezi mahitaji na kusababisha wakati wa mapumziko baadhi ya wanafunzi kujisaidia vichakani.

Hali hiyo imesababisha walezi na wazazi kuamua kuchangishana fedha ili kujenga matundu 24 ya vyoo kati ya 29 yanayohitajika kutatua kero hiyo.

Hayo yalibainishwa jana na wananchi wa kata hiyo katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika kijiji cha Ngokolo, ulioitishwa na Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Emmanuel Cherehani, kwa ajili ya kusikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi.

Mkazi wa Kijiji cha Ngokolo, Paskali Masanja, alisema matundu ya vyoo yaliyoko katika Shule ya Msingi Ngokolo hayatoshelezi mahitaji.

Alisema hali hiyo inawafanya wanafunzi kujisaidia vichakani.

Kwa upande wake, Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Jenifa Lucas, alisema wanafunzi wa shule hiyo wanapata shida kutokana na upungufu wa matundu ya vyoo.

Kwa upande wake, Mbunge Cherehani, aliwapongeza viongozi wa kata hiyo kwa kuendelea na shughuli za maendeleo.

Aliwaomba wananchi hao kumpatia bajeti ya ujenzi wa matundu ya vyoo ili aweze kuchangia.

Mpango wa kuinua wasichana ki-TEHAMA waja Afrika, ni mataifa 11



Ukurasa 13

Nipashe
TESA
Jumanne Mei 3, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

## Wajasiriamali Tanga, Pemba kuula mafunzo uwekezaji uchumi buluu

NA MWANDISHI WETU

NI SIKU YA UHURU WA HABARI

# Tasnia inavyovurugwa na uandishi wa kidijitali


Nipashe
TESA
Korti yaihoji Jamhuri kueleza sababu kesi ya Tundu Lissu kuchelewa
Serikali yaanika vipaumbele 13 vya ukuaji uchumi Mwaka wa Fedha 2021/22
Uchaguzi wa kombinesheni wamuibua Waziri mtandaoni
• Atumia muda kuwajibu kwa mifano, wengi waliojitokeza kueleza shida ziliko... Endelea Uk.2
Samia afuta mashamba, awagawia wananchi
Lowassa, Mbowe walivyomlilia TB Joshua
MICHEZO WACHEZAJI YANGA WAIANIKA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6


LEO ni Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani. Tasisi hizi zina jukumu kubwa la kuuhabarisha umma, kutoa sauti za wasiosikika, kutetea wanyonge na kuongeza msukumo kwenye serikali ili zilinde haki za binadamu, kudumisha amani, demokrasia na kuleta maendeleo.

Tasnia ya habari ni muhimu kwenye kila nyanja, kuanzia kwenye siasa, uchaguzi, huduma za jamii, vita, kilimo, sayansi na teknolojia na kwenye milipuko ya magonjwa ikiwamo kuwafikisha wananchi taarifa muhimu za kujikinga magonjwa ya milipuko ikiwamo corona.

Sekta ya habari leo na kesho itaendelea kuwa muhimu popote pale ili kukabiliana na zama za upotoshwaji wa taarifa. Mei 3, kila mwaka ni jukwaa la kuzikumbusha serikali na vyombo vya dola kulinda na kuheshimu uhuru na haki ya kupata habari pamoja na kuuthamini mchango wa wanahabari na vyombo vya habari.

Lakini ni wakati wa wanahabari kutafakari na kuangalia mwenendo mzima wa kazi zao, kuanzia ufanyaji kazi kwa maadili, changamoto, mafanikio na matarajio yao katika kuendeleza jukumu kubwa la kuuelimisha na kuuhabarisha umma ili kuuletea mabadiliko na maendeleo.

Kwa mujibu wa Shirika la Elimu Sayansi na Teknolojia la Umoja wa Mataifa (UNESCO), Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari inakwenda mbali zaidi kwa vile ni wakati wa jamii kuona namna bora ya kushirikiana na kuwaunga mkono wanahabari, taasisi zake pamoja na kuweka mazingira bora ya kufanyakazi.

Ni kwa kigezo hicho kuangalia na kuondoa sheria kandamizi zinazoumiza uhuru wa vyombo vya habari, zinaweka vikwazo vya ufanyakazi kwa wanahabari, faini, masharti na gharama kubwa dhidi ya tasnia ya habari.

UNESCO inasema Mei 3, ni wakati wa kuwakumbuka na kuwaenzi wafanyakazi wa tasnia ya habari waliopoteza maisha yao wakitafuta taarifa mbalimbali muhimu kwa ajili ya wasomaji, watazamaji na wasikilizaji wao.

"Kila mwaka Mei 3 ni siku kuadhimisha na kusimamia misingi ya uhuru na haki ya habari, kutathmini mafanikio na changamoto duniani. Kulinda na kuepusha mashambulizi dhidi ya uhuru wa vyombo vya habari na wanahabari na kuwakumbuka waliopoteza maisha yao..." inaongeza UNESCO.

### HISTORIA

Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani - World Press Freedom Day' ilianzishwa na UN mwaka 1993 kufuatia mapendekezo ya UNESCO ya kuwapo na umuhimu wa kipekee kuilinda, kuendeleza na kuithamini tasnia hiyo mwaka 1991.

Vuguvugu la kuwa na uhuru na ulinzi wa wanahabari na tasnia nzima ya upashanaji lilianzia Afrika mwaka 1991 baada ya wanahabari kutoa Azimio la Windhoek la kutaka kuwa na tasnia huru ya habari, yenye vyombo vingi, inayojitegemea na inayoundwa na wadau mbalimbali.

UNESCO inaamini kwenye uhuru wa kupata habari na kutoa taarifa kama msingi wa kujenga na kuwa na amani na maendeleo endelevu, hivyo katika maadhimisho hayo ni wasaa wa kuwaeleza wananchi kuhusu ukiukaji wa haki za uhuru wa wana habari.

Ni wasaa pia wa kutafakari jinsi madola yanavyoingilia uhuru wa vyombo vya habari, kufungia magazeti na vituo vya televisheni, redio, kuadhibu mitandao ya kijamii, kukatisha matangazo, kukata mitandao ya intanet na kuzuia mawasiliano kwenye mataifa yao.

Aidha, pamoja na figisu hizo, wapo waandishi, wahariri na wachapishaji walionyanyaswa, kufunguliwa mashtaka na kufungwa na hata kuuliwa kwa sababu ya kutekeleza majukumu ya kuuhabarisha umma.

UNESCO inasema Mei 3, kila mwaka ni siku ya kuwatia moyo na kuwahamasisha wana habari kufanyakazi zao kwa juhudi na maarifa na kimaadili zaidi.

Aidha, ni wakati wa kuongeza juhudi za kuimarisha uhuru wa habari duniani na kuangalia mwenendo mzima ulivyo duniani kote.

### UJUMBE MWAKA 2022

TANESCO inasema zama hizi uandishi na uhuru wa habari unakabiliwa na changamoto mbalimbali kubwa ikiwa ni kubanwa na kuzingirwa na uandishi wa kidijitali.

Kauli mbiu ya mwaka huu ya Siku ya Uhuru wa Habari ni "Uandishi wa Habari katika Dunia ya Kuzongwa na Uandishi wa Habari Kidijitali" ambayo inaainisha vitisho vipya kwa tasnia ya habari vinavyotokana na ukuaji wa teknolojia ya uandishi mitandaoni ambao unahitaji kukwamuliwa na wadau wote.

UNESCO inawataka wanaoandika kwenye mitandao ya kijamii kuongeza uwazi kuhusu taarifa zao, kudhibiti kusambaa taarifa za uongo na upotoshaji ili kulinda vyanzo vya habari vya kuaminika. Inasema uongozi unaolinda haki za binadamu unahitajika ili kuhakikisha kampuni na mtandao ya intaneti zinadhibiti taarifa za upotoshaji na uongo, chuki na maudhui yanayohatarisha amani.

"Hii ni lazima iendane na matakwa ya viwango vya kimataifa vya uhuru wa kujieleza, haki ya kupata habari na usalama na ulinzi wa wanahabari," inasema taarifa ya UNESCO.

Viwango vya kulinda faragha za watu lazima pia viimarishwe kutokana na ongezeko la kudukuliwa

INAENDELEA UK.14

ELIMU
NA GERALD KITABU

# Wajasiriamali Tanga, Pemba kuula mafunzo uwekezaji uchumi buluu




Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima (kushoto), akikabidhi mfano wa hundi kwa vikundi vilivyo na mawazo ya biashara kwenye uchumi wa buluu. Wengine ni maofisa mbalimbalii wanaofanikisha mpango wa kuendeleza wajasiriamali. **PICHA: GERALD KITABU**

SEKTA ya uchumi wa buluu ambayo kwa kiasi kikubwa hapa nchini inajihusisha na uvuvi ni eneo linaloelezwa kuwa linaweza kuwa mwarobaini wa kupunguza umaskini kwa wakazi wa ukanda wa pwani iwapo watapewa elimu, fursa na mitaji ili kubadili maisha yao.

Hata hivyo, utaalamu na mafunzo kuhusu uvunaji na uendelezaji rasilimali bahari haujafanyika kusaidia kikamilifu kusaidia wananchi kubadili maisha yao, kwani kwa miaka mingi jamii ya watu wa pwani imeendelea kutonufaika kikamilifu na fursa zilizoko na hivyo kutokuwa na kuimaraika kwa kasi kiuchumi.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima, anasema wakati wa kuzindua programu ya mafunzo na kukuza ujasiriamali wa uchumi wa buluu ukanda wa bahari wa Tanga na Pemba, kuwasaidia wajasiriamali kuwekeza na kuuza rasilimali za bahari kwa tija.

Katika programu hiyo Shirika la Kimataifa la International Union for Conservation of Nature (IUCN), ndilo linalohusika na kukuza ujasiriamali wa uchumi wa buluu ukanda wa bahari wa Tanga-Pemba.

Kwa kuanzia, programu itafanyakazi na vikundi kadhaa vilivyoandaa mawazo ya kibiashara yanayoonyesha kuwa na fursa kubwa zaidi ya kuleta matokeo chanya kwenye mazingira na maisha ya wananchi hasa kina mama na vijana.

> “Shirika la IUCN kwa kushirikiana na Taasisi ya Ocean Hub Africa (OHA) na Ubalozi wa Ireland nchini Tanzania, ndiyo watekelezaji wa mradi huo.

Vikundi vilivyochaguliwa vitafunzwa ujasiriamali na kupewa mtaji wa fedha wa takriban Sh. milioni 126 kukuza na kuongeza tija kwenye biashara zao.

Jifute ni kikundi kilichochaguliwa kunufaika na mpango huo wa IUCN, ambacho baada ya kusajiliwa 2021 kikiwa na wanachama wanawake na wanaume kimefanya ujasiriamali baharini katika Wilaya ya Pangani kwenye Kijiji cha Msaraza.

Wajasiriamali hao wanafuga na kunenepesha kaa wa bahari, kupanda upya ili kurejesha misitu ya mikoko iliyotoweka baada ya kukatwa na kuharibu mazingira ya bahari.

Wanachama hao wanasema majukumu yao mengine ni kuongeza thamani kaa hao na kuuza kwenye masoko mbalimbali.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Maneja wa Programu ya Ustahimilivu wa Pwani na Bahari Elinasi Monga, anasema programu hiyo inalenga kuleta matokeo chanya ya kimazingira, uchumi na kijamii yanayopatikana kwa kuwawezesha wajasiriamali wadogo kubuni na kufanya biashara zenye tija kiuchumi na kimazingira.

Shirika la IUCN kwa kushirikiana na Taasisi ya Ocean Hub Africa (OHA) na Ubalozi wa Ireland nchini Tanzania, ndiyo watekelezaji wa mradi huo.

Monga anasema kuwa programu hiyo inatetea utengenezaji na utekelezaji wa sera na mifumo ya fedha ambayo ni rafiki ili kuwezesha utekelezaji shirikishi wa sera ya uchumi wa buluu nchini (Bara na Zanzibar).

“Tunataka pia kuonyesha biashara za wajasiriamali wadogo katika uchumi wa buluu ambazo zinaweza kuwezeshwa na kuleta tija kiuchumi, kimazingira na kijamii,” anaongeza Monga.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima, anavisihi vikundi kushiriki mafunzo kikamilifu na kutumia fedha watakazopewa kwa malengo yaliyokusudiwa.

“Napenda pia kutoa maelekezo kwa wafanyakazi wa serikali katika sekta ya uvuvi kushirikiana na vikundi hivi ili kuhakikisha wanapata msaada wa kitaalamu ili viweze kufikia malengo yanayotarajiwa. Nafahamu kuna wawakilishi wa Sekretarieti ya Mkoa, naomba tuhakikishe programu hii inapata matokeo chanya ili kuvutia zaidi misaada ya namna hii kwa wananchi wetu,” anasema.

Anasema kuwa asilimia 40 ya Watanzania wanaishi ukanda wa pwani na kwa kiwango kikubwa wanategemea rasilimali bahari kwa ajili ya kuendesha maisha yao.

Urefu wa ukanda wa pwani ya bahari kutoka Tanga mpaka Mtwara ukiwa na mtawanyiko mkubwa wa mifumo ya ikolojia ya bahari na pwani inayotoa huduma na bidhaa mbalimbali za mifumo ya kiikolojia ni fursa mahsusi kwa maendeleo ya wananchi wa pwani, anaongeza Malima.

Anaongeza kuwa shughuli ya uvuvi mdogo, utalii wa pwani na ufugaji wa viumbe vya bahari ni sekta muhimu ambazo zinasaidia jamii kubwa kuendesha maisha yao na kuchangia uchumi wa nchi.

Malima anasema hata hivyo, kwa miaka mingi jamii ya watu wa pwani imeendelea kutonufaika kikamilifu na fursa zilizoko na hivyo kutokuwa kwa kasi nzuri kiuchumi.

“Changamoto hii inachangiwa na miundombinu hafifu hasa ya uvunaji, uchakataji, uhifadhi na usafirishaji wa mazao ya pwani na bahari, maarifa na ujuzi sahihi kwa wavuvi wadogo wadogo na ukosefu wa mitaji,” anasema Malima.

Anaongeza kuwa ili sekta ya uvuvi iweze kuleta tija zaidi ni lazima kuwawezesha wavuvi wadogo kuongeza ukubwa wa kazi zao na kufanya kazi hizo kwa kasi inayoendana na ukuaji wa mahitaji ya bidhaa na huduma za mazao ya bahari na pwani ndani na nje ya nchi.

Malima anasema ni kwa sababu uvuvi mdogo ni muhimili muhimu wa sekta hii ya uvuvi, ukichangia asilimia 98 ya samaki wanaovuliwa nchini na kuchangia pato ghafi la taifa kwa asilimia 1.3.

Aidha, uvuvi mdogo unachangia mpaka asilimia 9.9 ya samaki wanaosafirishwa nje ya nchi na kuingizia serikali mapato ya kigeni kiasi cha wastani wa Dolla za Kimarekani milioni 12.4, anasema Mkuu wa Mkoa wa Tanga.

Wakati takwimu hizi zikionyesha kuwa bado mchango wa sekta ya uvuvi katika maendeleo ya wananchi na nchi ni mdogo lakini sekta hiyo ni muhimu kwa kuwa ni chanzo kikubwa cha chakula

INAENDELEA UK.14

ELIMU
NA SABATO
KASIKA

# Mpango wa kuinua wasichana ki-TEHAMA waja Afrika, ni mataifa 11




Dk. Dorothy Gwajima (wasita kulia) na viongozi wengine walipozindua mpango wa kuzindua wasichana kwenye TEHAMA. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

TEKNOLOJIA ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ni moja ya nguzo muhimu ya uchumi imara unaojengwa na elimu bora katika zama hizi za sayansi na teknolojia.

TEHAMA licha ya kuunganisha watu kimawasiliano, inawezesha wanafunzi katika masomo na ujuzi wa fani za aina mbalimbali.

Licha ya umuhimu huo, inaelezwa kuwa nusu ya watu dunia hawajaunganishwa kwenye mtandao, wengi wa hao wanaokosa huduma ni wanawake, hasa wanaoishi kwenye mataifa yanayoendelea.

Kutokana na hali hiyo, serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuwezesha Wanawake na Kuleta Usawa wa Kijinsia (UN Women) na wadau wa maendeleo wanatarajia kuanzisha vituo vya mafunzo ya kidijitali kwa wasichana.

Ni kupitia mradi unaojikita kuongeza ushiriki kwa wasichana katika TEHAMA.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Doroth Gwajima, anabainisha hayo wakati akizindua awamu ya pili ya programu ya kuhamasisha wasichana Afrika kushiriki katika TEHAMA.

Uzinduzi huo unaofanyika Dar es Salaam, hivi karibuni, unahusisha nchi 11 za Tanzania, Msumbiji, Senegal, Mali, Kenya, Rwanda, DR Congo, Niger, Uganda, Afrika Kusini na Burundi ambazo kila taifa litakuwa na vituo viwili vya mafunzo.

Anasema, mradi huo utaandaa wanafunzi waliopo shuleni na wengine wanaopenda maendeleo ya kidijitali waweze kuendelea na mafunzo ya TEHAMA.

"Taratibu zote za kuwapo kwa vituo ikiwamo kuanza kwake, maeneo vitakapowekwa kwa upande wa hapa nchini na mambo mengine, tutatoa taarifa, kwani unahusisha wadau wengi ikiwamo Wizara ya Elimu," anasema Dk. Gwajima.

Waziri anasema, serikali imeridhia kutekeleza mikataba ya kimataifa na ya kikanda, ukiwamo wa kutokomeza ubaguzi wa aina zote wa mwaka 1978, Azimio za Beijing, mkataba wa kimataifa wa haki za mtoto wa mwaka 1989.

"Vilevile mpango wa maendeleo endelevu wa 2030, Ajenda ya Afrika Tunayoitaka ya mwaka 2063 na Mkataba wa Afrika wa Haki za Mtoto mikataba inayolenga kuhakikisha kunakuwa na usawa wa kijinsia," anasema.

> Mradi huu umejikita kuongeza ushiriki kwa watoto wa kike katika masuala ya teknolojia na Tanzania imepata fursa ya kuzindua na utatekelezwa kuanzia 2022 mpaka 2023.

Anasema, Watanzania wanayo kila sababu ya kuyafikia malengo hayo kwa kuzingatia muda uliowekwa, huku akiwasihi wasichana kujitokeza kwa wingi kujifunza na kubobea kwenye ujuzi na maarifa ya TEHAMA.

"Hivi sasa ili uweze kupata kazi, lazima uwe na uwezo wa kidijitali sasa je, wasichana au wanawake wetu wana uwezo huo? Jibu ni hapana na asilimia 90 za kazi zijazo zitahitaji uwezo wa kidijitali," anaeleza Waziri.

Anasema, hali hiyo inawasukuma kuja na mpango huo wa kuanzisha vituo hivyo kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ya elimu ambavyo anaamini vitasaidia uelewa wa wanafunzi wa kike kwenye TEHAMA.

### KUKOSA AJIRA

Aidha, Waziri Dorothy anasema utafiti unaonyesha kuwa asilimi 90 ya ajira kwa kipindi kijacho, zitahitaji ujuzi wa TEHAMA, na kwamba kuna haja ya kuwawezesha wasichana wengi kuwa na ushiriki kwenye teknoloijia.

Anasema, katika mazingira hayo, wanawake hawataonekana katika uongozi, ajira, maendeleo ya kiuchumi na kisiasa kwa kuwa dunia inaelekea kwenye dijitali.

"Ndiyo maana nasi tumekuja na mpango huu kusaidia wasichana kuingia katika soko, kwani hapo baadaye ajira zaidi ya milioni mbili zitakuwa katika nyanja ya kompyuta, lazima uwe na uwezo wa kuifahamu," anasema.

Mtaalamu wa kuwawezesha wanawake kiuchumi kutoka UN Women, Lilian Mwamdanga, anasema shirika hilo limeungana na Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AU) kuzindua mradi wa nchi 11 duniani.

"Mradi huu umejikita kuongeza ushiriki kwa watoto wa kike katika masuala ya teknolojia na Tanzania imepata fursa ya kuuzindua na utatekelezwa kuanzia 2022 mpaka 2023," anasema Lilian.

Anafafanua kuwa kuna kizazi cha usawa wa kijinsia ambacho pia Tanzania ni mwanachama wake, huku katika malengo maendeleo endelevu ya Umoja wa Mataifa mojawapo ni ushiriki wa wanawake katika fursa.

Lilian anasema, fursa hizo ni zile rasmi ili kwamba ushiriki wao uongezeke kupitia nyanja mbalimbali ikiwamo teknolojia na kwamba hatua hiyo itaongeza kasi ya utekelezaji wa maendeleo hayo.

### ZANZIBAR KUCHELE

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe Juma, anasema, kama ilivyo kwa Tanzania Bara, nao wamekuwa wakitoa kipaumbele kwa watoto wa kike.

"Tunafanya hivyo kupitia programu ya FAWE na FEMU, lakini kupitia vyuo vikuu vya Zanzibar na cha Karume, tunawawezesha wanawake wa vijijini kwenye programu za kisayansi," anasema Riziki.

Anataja mojawapo ya uwezeshaji huo kuwa ni utengenezaji wa taa zaa umeme wa jua, hasa kwa wale waliopo vyuoni na walio nje ya vyuo ili kuhakikisha wanapata ujuzi wa kuwawezesha kujiajiri.

Nao mabinti Thereza Joseph, kutoka Tanzania na Fatou Ndiaye kutoka Senegal waliokuwa wakisomea fani ya TEHAMA, wanapongeza juhudi zinazochukuliwa katika nchi za Afrika kuwezesha watoto wa kike kupata elimu ya ujuzi mbalimbali.

"Kwa msukumo huu uliowekwa na serikali zetu, utamwezesha msichana kufikia malengo yake, kwani jamii nyingi za kiafrika zilikuwa hazitoi kipaumbele kwa watoto wa kike kwenye suala la elimu, lakini sasa kwa mwamko huu, tunaiona kesho yetu,' anasema Thereza.

# Wajasiriamali Tanga, Pemba kuula mafunzo uwekezaji uchumi buluu

INATOKA UK.12

na ajira kwa wananchi wengi wa pwani, anaongeza MKuu wa Mkoa.

"Programu hii ya kukuza ujasiriamali wa uchumi wa buluu ambayo imezinduliwa hapa ni ubunifu kwasababu inakwenda kutoa majibu ya changamoto kadhaa zinazowakabili wavuvi wadogo. Majibu hayo ni pamoja na kuwajengea wananchi uwezo kwa njia ya mafunzo na mitaji ili kukuza biashara zao," anasema Mkuu wa Mkoa.

Meneja programu anayeshughulikia mazingira na mabadiliko ya tabianchi ubalozi wa Ireland Fazal Issa anasema kuwa Ireland inafahamu umuhimu wa rasilimali za bahari na fukwe na mfumo wa ikoloji kwa wananchi.

Umuhimu huo unajumuisha kuimarisha usalama wa chakula, kutoa fursa ya kuingiza kipato, na kukuza uchumi. Ingawa kuna faida nyingi, jamii za maeneo ya pwani na rasilimali hizo za bahari na fukwe zinakabiliwa na chagamoto kadhaa, anasema.

Hizi zinajumuisha uvuvi usioendelevu, uharibifu wa matumbawe, uchafuzi wa mazingira, kuongezeka kwa asidi baharini, na athari nyingine zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi ikiwamo kuongezeka kwa joto.

Hivyo, anasema programu hiyo ya kukuza ujasiriamali wa uchumi wa buluu ni muhimu katika kuboresha maisha ya jamii zinazoishi maeneo ya pwani na pia katika kulinda na kutunza ikolojia ya bahari.

"Hii ni moja ya sababu za Ireland kusaidia shirika la IUCN kutekeleza mradi wa uchumi wa buluu katika eneo la bahari la Tanga-Pemba, ambapo programu hii ya Kukuza Ujasiriamali wa Uchumi wa Buluu (Blue Economy Incubation Program) ni sehemu muhimu ya mradi huo," anasema Issa.

Uchumi wa buluu, uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, na uwezeshaji wa wanawake ni maeneo ya kipaumbele katika Sera ya Maendeleo ya Kimataifa ya Ireland inayoitwa A Better World au dunia au Dunia iliyo Bora, anasema Issa.

"Vipaumbele hivi pia vimejumuishwa katika Mpango Mkakati mpya wa miaka mitano wa Ubalozi wa Ireland nchini Tanzania. Katika Mpango Mkakati huu mpya wa Ubalozi, kipaumbele cha Ireland katika kufanya kazi na wanawake kitaendelea na kuimarishwa zaidi." Anasema Issa.

Anaongeza: "Sambamba na kipaumbele hiki, Ireland itaimarisha kazi katika uhimili wa mabadiliko ya tabianchi ikiwamo maendeleo ya uchumi wa buluu. Masuala ya usawa wa kijinsia na uhimili wa mabadiliko ya tabianchi yana uhusiano mkubwa." Anaongeza.

# Tasnia inavyovurugwa na uandishi wa kidijitali

INATOKA UK.11

kwa taarifa na mienendo binafsi ya watu inayofanyika kutokana na ukuaji wa teknolojia unaopelekea wizi wa taarifa mitandaoni, kushikilia taarifa, ujasusi wa kimtandao na ufuatiliaji na udukuzi wa haramu wa taarifa za wanahabari.

UNESCO inakumbusha kuwa katika maadhimisho hayo, hatua za kisheria zinahitajika kulinda wanahabari na kukomesha ufuatiliaji haramu wa waandishi wa habari,

Aidha, inakumbusha umma na sekta binafsi, kuimarisha ulinzi wa kisheria wa waandishi wa habari na kusimamia utunzaji siri na vyanzo vya taarifa zao.

Halikadhalika inayakumbusha majukwaa mbalimbali na kuchukua hatua kali ili kuzuia na kuondoa mashambulizi ya mtandaoni dhidi ya wanahabari, kampeni zilizoratibiwa za unyanyasaji, vitisho na ukiukaji wa faragha zao.

Pia inataka hatua madhubuti zinafaa zichukuliwe ili kuwalinda wanahabari wanawake, ambao wanalengwa na kuchafuliwa mtandaoni na nje ya mitandao ili kukabiliana na mashambulizi ya mitandaoni kwa kundi hili.

UNESCO inataja changamoto nyingine ya kukabiliana nayo kuwa ni kulinda uchumi wa wa vyombo vya habari, kwa sababu vingi vinaendelea kuwa taabani kutokana na mapato yake kuporwa na utangazaji unaofanywa kwenye mitandao, na kusababisha janga la ukosefu wa mapato na uchumi kuyumba kwa tasnia hiyo ambacho ni kitisho kinachoelekea kuporomosha uhuru na uwepo wa vyombo vingi vya habari duniani.

Inayakumbusha mataifa, mashirika ya kijamii, kampuni za mitandao na kiraia wote kuwa wana jukumu la kuviokoa vyombo vya habari kuzingira pamoja na kubanwa na uandishi wa kidijitali. Shirika hilo linawashauri kutafuta suluhu na kuwa na maamuzi ya kudumu ya kumaliza tatizo hilo.

Mwaka huu Siku ya Uhuru wa Habari Duniani inazungumzia juu ya kutekeleza Azimio la Windhoek kwa vitendo ili kusaidia kupata taarifa kwa manufaa ya umma ambalo ni moja ya mahitaji muhimu na kama urithi kwa vizazi vijavyo.

## WANENAVYO MALENGA

### HOSPITALI NI TAMU?

Sijataka kufahamu, eti sababu ni nini?
Ila nimepata hamu, kujadili akilini,
Sipitali nafahamu, imeyeyuka porini,
Sijui tufurahie, au ndio sikitiko?

Sipitali nafahamu, njia panda ya chuoni,
Tulipotoa salamu, kwa magonjwa ya mwilini,
Sasa bango limetimu, imeingia mitini,
Sijui tufurahie, au ndio sikitiko?

Maswali ya ufahamu, kwangu yaleta kwa nini,
Magonjwa kwa binadamu, sasa yameshuka chini?
Ushindani wa kitimu, wateja sasa kapuni?
Sijui tufurahie, au ndio sikitiko?

Kuna baa nafahamu, iliyofungwa mjini,
Chereko kwa binadamu, ulevi kuwa kapuni,
Kwa wengine hilo gumu, bia hazipatikani,
Sijui tufurahie, au ndio sikitiko?

Hili swali ni muhimu, lafaa kwa mtihani,
Hosipitali ni tamu, au kwamba tu shidani?
Ongezeko tabasamu, magonjwa yawe pomoni?
Sijui tufurahie, au ndio sikitiko?

Natamani niwe zamu, kwa jibu la mtihani,
Nilitoe jibu tamu, sote tuwe furahani,
Kituo hakijadumu, no wagonjwa mtaani,
Sijui tufurahie, au ndio sikitiko?

Sipitali nazidumu, kule waliko shidani,
Lakini ziwe adimu, kusikowagonjwa ndani,
Kuzalisha wanadamu, ziwe karibu njiani,
Sijui tufurahie, au ndio sikitiko?

Afya zetu ziwe ngumu, na nguvu za kusheheni,
Sipitali tusidumu, kwenda kama ni kazini,
Mara chache chache humu, ndipo tuende wodini,
Sijui tufurahie, au ndio sikitiko?

Kwa mahitaji muhimu, mijini na vijijini,
Majengo mengi muhimu, kwa kweli yamesheni,
Hata dawa za muhimu, nyingi ziko kabatini,
Sijui tufurahie, au ndio sikitiko?

Ile kazi kujihimu, watalamu kuwa ndani,
Hiyo kwa sasa muhimu, sote tuwe furahani,
Hatua za sasa tamu, tutafika kileleni,
**Sijui tufurahie, au ndio sikitiko?**

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

### KIWANDA CHA MSAADA

Kiwanda cha msaada, lazima kifilisike,
Kinazalisha kwa ada, gharama na zikitoke,
Eti iwe kawaida, ofa nyingi na zitoke,
Sipo hesabu gharama, umekwisha umechacha.

Kiwanda cha msaada, ni lazima kianguke,
Nguvu ni povu la soda, ni lazima ziyeyuke,
Watu wale mabumunda, mshumaa uyeyuke,
Sipohesabu gharama, umekwisha umechacha.

Kiwanda cha msaada, umeme na utumike,
Na tena muda kwa muda, maji mengi yamwagike,
Watendaji kama ada, jasho jingi liwatoke,
Sipohesabu gharama, umekwisha umechacha.

Kiwanda cha msaada, nje na kifahamike,
Endapo kuna kigoda, kukinadi kitumike,
Na juisi za kugida, kinywe hadi zimwagike,
Sipohesabu gharama, umekwisha umechacha.

Kiwanda cha msaada, kikifa tukikumbuke,
Maisha yenye ziada, machoni na yafutike,
Ibakie kawaida, historia tucheke,
Sipohesabu gharama, umekwisha umechacha.

Malighafi wewe oda, hata tenda zifanyike,
Mtaji ule wa muda, leta wote utumike,
Zalisha kikawaida, na bidhaa zigawike,
Sipohesabu gharama, umekwisha umechacha.

Kiwanda cha msaada, maneno uyaandike,
Hata kama wewe kada, hapo bora uondoke,
Kwani itafika muda, msukule utumike,
Sipohesabu gharama, umekwisha umechacha.

Kiwanda cha msaada, vizuri kieleweke,
Sasa igeuze mada, kwingine na utumike,
Uone kama ni ada, misaada iwatoke,
Sipohesabu gharama, umekwisha umechacha.

Hii methali ya muda, ni lini ieleweke?
Kazi fanya kawaida, kumbukumbu siandike,
Eti uone faida, na kiwanda kiinuke?
Sipohesabu gharama, umekwisha umechacha.

Kiwanda cha msaada, kiache kipukutike,
Hadi akili ziada, kwenye kichwa ikufike,
Kwenye kaburi mashada, mengi mengi tuyaweke,
Sipohesabu gharama, umekwisha umechacha.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**



## Mhagama: Bahi msikope fedha kufanya sherehe

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Jenista Mhagama, amewataka wakazi wa Kata za Msisi na Makanda wilayani Bahi kutotumia hati za mashamba kukopa fedha kwa ajili ya sherehe badala yake wafanye maendeleo ili kujiinua kiuchumi.

Mhagama alitoa angalizo hilo katika ziara ya kikazi ya kutembelea kata hizo ambapo aligawa hati za mashamba 2,890 ambazo zimerasimishwa kwa wakazi

wa kata hizo kupitia Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA).

Alisema kugawiwa kwa hati hizo na serikali wanahesabika kama wawekezaji, hivyo watumie fursa walionayo kukopa katika benki ili kufanya maendeleo na kujiinua kiuchumi.

Alifafanua kuwa asingependa kusikia wametumia hati kukopa fedha katika Benki za NMB, CRDB na nyinginezo kwa ajili ya kwenda kufanya sherehe bali anapenda kusikia wamekopa ili kuendeleza kilimo biashara.

"Kukabidhiwa hati tayari mmekuwa wawekezaji, tumieni hati zenu kukopa ili kuendesha kilimo chenye tija," alisema Mhagama.

Alisema serikali imejipanga kuhakikisha inaleta mageuzi katika sekta ya kilimo, hivyo itatumia hati walizonazo kuwaunganisha kufanya kilimo cha mtama mfupi na alizeti, ambavyo vyote vina soko ndani na nje ya nchi.

Aliwataka wakazi wa kata hizo kuweka jitihada za kuhakikisha wanarasimisha mashamba waliyonayo ili kuwa na uhakika na hati ambazo zitawasaidia kuchukua mikopo na kutengeneza vitega uchumi.

Akielezea baadhi ya faida ambazo watazipata baada ya kurasimisha mashamba yao na kukabidhiwa hati, alisema unyanyasaji wa kijinsia utapungua, wataishi kwa amani kwa sababu hati za umiliki wa mashamba yao wanazo, ambazo zinawasaidia kwenda kukopa benki kwa ajili ya kuendeleza kilimo biashara ambacho kinaleta tija.

Aliiagiza MKURABITA kuhakikisha masijala walizojenga zinafanya kazi kwa weledi ya kutunza kumbukumbu za hati ambazo zimetolewa ili kuepusha migogoro kwa wanakijiji wa maeneo hayo.

Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Mukunda, alisema wilaya hiyo imepata bahati kubwa ya wakazi wake kurasimishwa hati za mashamba yao kutokana na kwamba wanakwenda kuinuka kiuchumi.

# Shekhe ataka yatima, wajane, wenye mahitaji wasaidiwe

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHEKHE wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, amesema kusaidia yatima, wajane na watu wenye mahitaji maalum isiwe wakati wa kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani pekee bali iwe ni sehemu ya maisha ya kila siku ya Watanzania.

Shekhe Rajabu alibainisha hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Alisema Mwezi wa Ramadhani unapaswa kutumika kwa Waislamu kama semina elekezi ya kuwasadia kuendelea kufanya mambo mema katika miezi mingine 11.

"Kusaidia yatima na wajane isiwe tuu wakati wa mfungo wa Ramadhani bali iwe kila sku kwani Mungu yupo kila mwezi na kila wakati kwani na wao ni binadamu wanamahitaji kama ilivyo kwa wengine,"alisema.

Aidha, aliwatakana Watanzania kuendelea kushikamana na kulinda amani na utulivu ulioko nchini pamoja na kumwombea Rais Samia Suluhu Hassan. "Lazima tumwombee Rais aweze kuongoza Taifa letu vizuri, kiongozi wa nchi akitengemaa na taifa lake litatengemaa kama ilivyo kivuli cha mti ukipinda na kivuli chake lazima kitapinda tuu,"alisema.

Kadhalika, alimpongeza Rais kwa kuzindua Filamu ya Royal Tour, na kuwataka Watanzania kumpa ushirikiano katika azma yake ya kuifungua nchi kiutalii.

Alisema wanaobeza jitihada za Rais wanapaswa kupewa elimu ili kujua umuhimu wa jambo hilo.

"Hatupaswi kuwapuuza bali tunatakiwa kuwaelimisha ili wajue umuhimu wa jambo hilo na kuacha kubeza jitihada za mweshimiwa Rais,"alisema.

Akizungumzia sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23, alisema kila mtu anapaswa kushiriki kikamilifu ili kuiwezesha serikali kupata takwimu sahihi.

"Hata katika imani jambo la sensa ni la muhimu sana kwani kuhesabiwa kwetu ndiko kunatuwezesha kujua tuko wangapi lakini kati yetu walemavu wangapi, wazee wangapi, wagonjwa wangapi ili serikali iweze kutuhudumia kulingana na idadi yetu," alisema.

Vilevile, alisema kutokana na uhaba wa mvua unaotishia ukame katika msimu huu wa kilimo wananchi wanapaswa kutunza chakula ili kukabiliana na baa la njaa linaweza kujitokeza.

"Tuchukue tahadhari ulichonacho kibane na kuacha kutumia chakula kwa matumizi mengine yasiyokuwa na tija hata majumbani kwetu tule kama alivyoagiza Mtume wetu kula njaa inapouma siyo kula kula ovyo," alisisitiza.




Mfanyakazi wa Manispaa ya Ubungo, Francis Vicent, akiweka namba kwenye nyumba (anwani za makazi) katika kata ya Manzese mtaa wa Kilimani mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Madiwani wafundwa kusoma taarifa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, amewataka madiwani kuwa na tabia ya kusoma mara kwa mara taarifa zinazotolewa na wataalamu kupitia vishikwambi vyao badala ya kusubiri vikao.

Ushauri huo ulitolewa baada ya baadhi ya madiwani kuuliza maswali ya kufuatilia miradi mbalimbali iliyoko ambayo majibu yake yalishatolewa kupitia vishikwambi walivyonavyo. Mafuru akizungumza kwenye kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani kilichofanyika mwishoni mwa wiki, aliwataka madiwani hao kuwa na tabia ya kusoma taarifa kupitia vishikwambi hivyo ili waweze kuepukana na kuuliza maswali ambayo yameshajibiwa.

"Ndugu zangu waheshimiwa madiwani hivyo vishikwambi mlivyonavyo muwe mnasoma mara kwa mara kwa kuwa maswali mnayouliza majibu yake yameshajibiwa badala ya kuulizia kwenye vikao kama hivi.

"Nawaomba muwe na tabia ya kusoma kwa lengo la kutaka mpate taarifa za shughuli mbalimbali zinazofanyika kwa kuwa msiposoma mnaweza kujikuta mkiangalia katuni tu,"alisema.

Alisema kuwa vishikwambi hivyo vimekabidhiwa kwa madiwani na baadhi ya wakuu wa idara, ili wafuatilie taarifa za shughuli zinazofanywa za Halmashauri ya Jiji ikiwamo miradi iliyokamilika na ile inayoendelea kwenye hatua mbalimbali.

Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, aliwataka madiwani kuendelea kusimamia miradi waliyonayo kwenye kata zao ili halmashauri iweze kupata mapato.

Alisema mafanikio ya makusanyo ya mapato yapo mikononi mwa madiwani ambao ni wasimamizi wakubwa, hivyo wanatakiwa kuisimamia ili halmashauri iweze kupata mapato yake.



# CHADEMA yataka wanaharakati kuungana kudai Katiba Mpya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimewataka watumishi wa umma kuungana na wanaharakati wanaodai Katiba Mpya ili kuboresha mifumo ya upatikanaji wa haki na maslahi yao ikiwamo kupandishwa madaraja na nyongeza ya mishahara.

Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Tundu Lissu, aliyasema hayo juzi alipohutubia Kongamano la Vijana wa chama hicho Wilaya ya Mbeya Vijijini, lililokuwa na lengo la kuungana na wafanyakazi kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani.

Kiongozi huyo alihutubia kongamano hilo kwa njia ya mtandao akiwa nchini Ubelgiji ambako anaishi kwa zaidi ya miaka mitano tangu alipokwenda kutibiwa baada ya kujeruhiwa kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana jijini Dodoma. Alisema mifumo iliyoko sasa inawafanya watumishi wa umma kuwa ombaomba kwa maelezo kuwa kila mwaka wanapoadhimisha siku ya wafanyakazi madai yao yanakuwa ni yaleyale ambayo hata hivyo hayatekelezwi na serikali.

Alisema kutokana na mifumo ya kikatiba ya sasa hivi, nyongeza ya mishahara na kupandishwa madaraja kwa watumishi inakuwa kama hisani ya Rais aliyeko madarakani badala ya kuwekwa wazi kwenye katiba ya nchi.

"Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani kwa nchi yetu imekuwa kama siku ya kujinufaisha kisiasa kwa viongozi wa nchi badala ya kujibu hoja na mahitaji ya wafanyakazi kama ilivyo chimbuko la siku hii, sasa nawashauri watumishi waungane na wanaodai Katiba Mpya," alisema Tundu Lissu.

Alisema alimsikia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan akieleza kwamba 'lile jambo letu bado lipo' lakini hakuweka wazi jambo lenyewe.

Lissu alisema yapo mataifa jirani ya Tanzania ikiwamo Kenya ambayo haki na maslahi ya watumishi wa umma yameelezwa kwenye katiba yao na kwamba ndiyo sababu mishahara ya watumishi imekuwa ikipandishwa.

Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa chama hicho Taifa (BAVICHA), John Pambalu, aliiomba serikali kuwafutia kesi wafuasi wa chama hicho ambao wanakabiliwa na kesi kwenye mahakama mbalimbali nchini kwa maelezo kuwa wengi kesi zao ni za kutungwa.

Alisema chama hicho pamoja na vyama vingine vya upinzani vimepitia wakati mgumu katika kipindi cha zaidi ya miaka saba sasa kutokana na Katiba kuwa na upungufu ambao unampa mamlaka makubwa rais wa nchi.

Alisema katika kipindi hicho vyama vya upinzani havikuruhusiwa kufanya mikutano ya siasa, kuandamana wala kutafuta wanachama vitu ambavyo alisema vinatakiwa kufanyika kwa mujibu wa Katiba.

"Rais Samia alisema anataka kuanza ukurasa mpya wa kisiasa, sasa tunamwomba awafutie wafuasi wetu ambao wameshtakiwa kwa kesi za 'michongo' (kubambikwa) na wengine wanatumikia vifungo magerezani, tunaomba alifanye hili ili ndiyo tuanze ukurasa mpya," alisema Pambalu.

Mwenyekiti wa CHADEMA Jimbo la Mbeya Mjini, John Mwambigija, alisema pamoja na madhira yote ambayo chama hicho kimepitia, lakini bado kipo imara na kinaendelea na majukumu yake ya kisiasa. Aliwapongeza vijana wa chama hicho kwa kuendelea kuwa na misimamo ambayo imekifanya kuendelea kuwa na wafuasi katika maeneo yote nchini.



Mkazi wa Kijiji cha Mpakani Kata ya Ndandalo wilayani Kyela ambaye ni mmoja wa walioathirika wa mafuriko akikusanya matofali mwishoni mwa wiki kwa ajili ya kuanza upya ujenzi wa nyumba yake kutokana na kubomoka. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

## Madiwani waridhia Tukuyu kurudishwa kuwa kijiji

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, limeridhia kuvunjwa kwa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Tukuyu na kuurejesha kuwa kijiji baada ya kubaini hakuna mabadiliko yoyote kwa zaidi ya miaka 10 tangu mji huo ulipopewa hadhi hiyo.

Madiwani hao walifanya uamuzi huo mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha kawaida cha baraza hilo na kati ya kata nane zinazounda mji huo ni diwani wa kata moja pekee aliyekubali mji huo kuendelea kuwapo.

Diwani wa Kata ya Ikuti, Lusekelo Mwakibinga, alisema matarajio yao wakati wanaunda mamlaka hiyo ilikuwa ni kupata mji kamili baada ya miaka 10, lakini mpaka sasa hawajafikia hadhi hiyo kutokana na kutotokea kwa maboresho ya aina yoyote.

Alisema kwa sasa serikali inakusudia kuwaondoa watendaji wanaofanya kazi kwenye vitongoji vilivyoko vya mamlaka hiyo kutokana na sheria za serikali za mitaa kutoruhusu watumishi hao kukaa kwenye vitongoji.

Alisema kutokana na hali hiyo wanahisi wananchi watakosa baadhi ya huduma muhimu huku akieleza kuwa wamekuwa wakilalamikia baadhi ya mambo kutokuwa sawa.

"Endapo tungepata Mamlaka ya Mji kamili vitongoji vilivyoko vingegeuka kuwa mitaa, sasa sisi tumeona ni vema turejeshe kwenye kijiji ili tujipange upya," alisema Mwakibinga.

Diwani wa Kata ya Msasani, Robin Mwakapesa, alisema mpaka sasa wananchi wa Tukuyu Mjini wanapata huduma kama watu wa mjini wakati mji huo bado haujafikia hadhi hiyo.

Alisema katika maeneo ya vijijini, umeme unaounganishwa na Wakala wa Umeme Vijijini (REA) gharama yake ni Sh. 27,000 lakini wananchi wa Mji huo wanatozwa zaidi ya Sh. 300,000 jambo ambalo alisema ni kero.

Mwanasheria wa Halmashauri ya Rungwe, Geofrey Pondo, alisema kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa, madiwani wana mamlaka ya kufuta Mji kama ambavyo walipendekeza.

# Wafugaji waomba ruzuku dawa za mifugo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAFUGAJI wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wameiomba serikali kuweka ruzuku kwenye dawa za mifugo kama inavyokuwa kwenye sekta zingine ili kupunguza gharama za dawa hizo na vitu vingine vinavyotumika kwenye sekta hiyo.

Walitoa ombi hilo juzi jijini hapo wakati wa mkutano maalumu wa wadau wa ufugaji uliokuwa na lengo la kupitia Sera ya Mifugo ya mwaka 2006 na kusema gharama za pembejeo zinazotumika kwenye mifugo ni kubwa.

Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika cha wafugaji wa Ranchi ya Matebete wilayani Mbarali, Lokordu Siloma, alisema Sera ya Mifugo ya mwaka 2006 imepitwa na wakati katika baadhi ya vipengele kikiwamo kinachoeleza kuhusu nyanda za malisho.

Alisema kwa sasa dunia inakabiliwa na mabadiliko ya teknolojia, lakini sera ya ufugaji bado ina mambo yaleyale ya zamani licha ya kinachofanyika inakuwa kama sera ilisharekebishwa.

Alisema wafugaji wanasisitizwa kupunguza mifugo ili inayobakia iongezewe thamani, lakini hawasaidiwi ipasavyo namna sahihi ya kuiboresha mifugo hiyo kwenye maeneo yao.

"Wakati wa ukame wafugaji tunapoteza mifugo mingi sana, sasa tunahamasishwa kupunguza mifugo ili iendane na maeneo yetu ya ufugaji, tunashauriwa pia kuiongezea thamani mifugo yetu ili kupata tija, lakini hatusaidiwi kupunguza gharama za pembejeo," alisema Siloma.

Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika cha Mwamala wilayani Rungwe, Asha Lukasa, alisema miongoni mwa gharama zinazowatesa wakulima ni kuhimilisha mifugo ambayo alisema ni gharama kubwa kuliko kama wangewekewa ruzuku.

Alisema kwa sasa wanahimilisha ng'ombe mmoja kwa Sh. 35,000, lakini kungekuwa na ruzuku ya serikali gharama ingefikia Sh. 10,000 ambayo inaweza kuwa rafiki kwa wafugaji wa aina zote. Alisema wafugaji wengi wanashindwa kuboresha mifugo yao kutokana na gharama za uendeshaji kuwa juu hali aliyosema inawafanya wafugaji kupata tija ndogo.

"Sisi Rungwe sasa hivi tunamshukuru Mungu soko la maziwa yetu lipo zuri sana, tatizo linalotusumbua ni gharama za kuhimilisha ambazo ni kubwa mno, tunaomba maboresho ya sera hii yatuwekee ruzuku ya pembejeo kama ilivyo kwenye kilimo," alisema Asha.

Akifungua mkutano huo wa wadau, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Angelina Lutambi, alisema pamoja na upungufu iliyonayo Sera ya Mifugo ya mwaka 2006 imechangia maboresho mbalimbali ya sekta hiyo ikiwamo ongezeko la mchango wa sekta ya mifugo kwenye pato la taifa. Lutambi alisema kabla ya mwaka 2006 sekta ya mifugo ilikuwa inachangia wastani wa Shilingi trilioni moja kwenye pato la taifa, lakini kwa sasa inachangia Sh. trilioni 10.6.

"Lakini mifugo imeongezeka sana kutokana na utekelezaji wa sera hii, mwaka 2006/2007 ng'ombe walikuwa milioni 10.6 lakini kwa sasa wamefikia milioni 33.9 haya ni mafanikio makubwa sana kwenye sekta hii," alisema Dk. Lutambi.





# Watakiwa kuorodhesha maeneo yenye changamoto ya mazingira

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ameuagiza uongozi wa Idara ya Mazingira Zanzibar, kuorodhesha maeneo yote yenye changamoto ya mazingira ili kupatiwa ufumbuzi.

Hemed aliyasema hayo wakati wa hafla ya utiaji wa saini ujenzi wa daraja eneo la Sipwese lililoko Mtambile Kusini Pemba, hafla iliyofanyika Baraza la Wawakilishi Chukwani, Zanzibar.

Alisema Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeonyesha dhamira yake ya kusaidia kumaliza tatizo la mazingira na ameiomba Idara ya Mazingira kukamilisha orodha ya maeneo yenye changamoto ili kusaidia kutoa mwelekeo wa kuanza kazi hiyo kwa maeneo mbalimbali.

Alisema kuanza kwa ujenzi wa eneo kutasaidia kumaliza changamoto inayowakabili wananchi wa eneo hilo ikiwamo kuvuka kutoka sehemu moja kuelekea sehemu nyingine, changamoto ambayo ni ya muda mrefu.

Alisema, hatua iliyofikiwa ya kusaini ujenzi huo ni katika matunda ya ushirikiano baina ya pande mbili za Muungano hatua ambayo Wazanzibari wanajivunia.

Aidha, aliushukuru uongozi wa Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu wa kuwasaidia Wazanzibari na kumtaka mkandarasi wa mradi huo kuhakikisha anajenga kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa kwa malslahi ya wananchi wanaoishi eneo hilo na maeneo jirani.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Abdallah Hassan Mitawi, alisema kuwa chimbuko la ujenzi wa eneo hilo ni kupitia ziara ya aliyekuwa Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano, Mussa Zungu, aliyoifanya mwaka 2019 na kuahidi kusimamia ujenzi wa eneo hilo.

Alisema ujenzi huo ambao utagharimu Sh. bilioni 1.1, utachukua muda wa miezi 18 kukamilika.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Thabit Idarous Faina, alisema ujenzi wa eneo hilo utasaidia changamoto inayowakabili wananchi wa eneo la Sipwese ikiwamo kuvuka kutoka sehemu moja kwenda nyingine, maji ya chumvi kuingia katika eneo la kilimo pamoja na kupungua kwa eneo la makazi ya wananchi.

## Wakazi Zanzibar kusherehekea Siku ya Wafanyakazi Mei 8

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Vyama Huru vya Wafanyakazi Zanzibar (ZATUC), limesogeza mbele maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani Mei Mosi hadi wiki ijayo Mei 8, kwa ajili ya kutoa nafasi wafanyakazi wengi kukamilisha mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani pamoja na kusherehekea sikukuu ya Eid el fitry.

Katibu wa Shirikisho la vyama huru vya wafanyakazi Zanzibar, Khamis Mwinyi, akizungumza na waandishi wa habari, alisema wamelazimika kusogeza mbele maadhimisho hayo baada ya kuangukia katika matukio mawili muhimu yanayoigusa idadi kubwa ya wadau wao.

Alisema maadhimisho ya siku ya Mei Mosi yameangukia katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani wakati wafanyakazi wengi ikiwamo asilimia kubwa waumini wa dini ya Kiislamu Zanzibar, wapo katika mfungo huo ambao ni sehemu ya ibada muhimu.

"Tumeona ni bora kusogeza mbele maadhimisho ya siku ya wafanyakazi duniani hadi wiki ijayo tarehe 8, Mei hapo katika viwanja vya Maisara kwa ajili ya kutoa nafasi kwa wadau wetu ambao ni wafanyakazi kufanya maandalizi ya sikukuu ya Eid el Fitry vizuri," alisema.

Mapema Mwinyi alichukua nafasi hiyo kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa busara zake pamoja na uongozi wake uliojikita katika kuimarisha amani na utulivu.

Alisema tangu kuchaguliwa kuongoza Zanzibar, amefanya kazi kubwa ya kuviunganisha vyama vya siasa na hatimaye kuunda serikali ya umoja wa kitaifa ambayo imeimarisha amani na utulivu.

Aidha, alisema katika kipindi cha mwaka mmoja amefanya kazi kubwa ya kujenga mazingira mazuri katika sekta ya uwekezaji kwa kujenga mazingira mazuri hatua ambayo imewavutia wawekezaji wengi kuwekeza na hivyo kutoa matumaini makubwa ya kuongeza ajira.

"Shirikisho la vyama huru vya wafanyakazi (ZATUC) tunachukuwa nafasi ya kumpongeza Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa uongozi wake wenye busara ambao katika kipindi cha mwaka mmoja umefanya kazi kubwa ikiwemo kuzungumza na wafanyakazi katika kada mbalimbali kwa ajili ya kufahamu utendaji wao na kupokea changamoto za kazi," alisema.




Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omari Said Shaaban (kushoto), akisalimiana na Ofisa Mkuu wa Wateja Wakubwa na Serikali wa Benki ya NMB, Alfred Shao, katika hoteli ya Golden Tulip kisiwani Zanzibar walipokutana kwa ajili ya futari iliyoandaliwa na benki hiyo. Wengine ni Ofisa Mkuu wa Mikopo wa NMB, Daniel Mbotto (kulia), Mkaguzi Mkuu, Benedicto Baragomwa (katikati) na wapili kushoto ni Meneja Mwandamizi wa Mikopo ya Wateja Wadogo, Ally Ngingite. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SMZ, Hairu Engineering kujenga kiwanda cha maboti

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imetiliana saini hati ya ushirikiano na kampuni ya Hairu Engineering ya nchini Sri Lanka katika sekta ya uchumi wa buluu ikiwamo ujenzi wa kiwanda cha kutengenezea maboti za uvuvi.

Akizungumza katika hafla ya utiaji saini huo, Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Masoud Makame, alisema ni kielelezo moja wapo cha mwenendo na mwelekeo wa kubadilisha Zanzibar kiuchumi.

Alisema kukamilika kwa miradi hiyo katika suala la uchumi wa buluu na mazao ya baharini itakuwa ni moja kati ya eneo kubwa na tegemezi katika uchumi wa Zanzibar.

Alisema wakati huu jicho la serikali na sera ya Zanzibar ni uchumi wa buluu na wanategemewa na serikali kubadilisha uchumi wa Zanzibar na maisha ya Wazanzibari.

"Miradi hii ikikamilika basi itakuwa ni moja ya kichocheo kikubwa cha uchumi wetu na dhana ya uchumi wa buluu tutaanza kuiona kupitia miradi hii," alisema.

Alisema kukamilika kwa miradi hiyo ndani ya miezi sita ni jambo la faraja kuona inakwenda kwa haraka kama serikali inavyotaka.

Waziri Masoud alisema kukamilika kwa miradi hiyo kutatoa ajira zisizopungua 450 na kuzalisha ajira zaidi ya 1000.

Aidha, alipongeza hatua ya kupatiwa mafunzo ambayo yatatanua wigo kwa wazawa na tatizo kubwa lililokuwapo Zanzibar ni taaluma ya kufikia shughuli za uvuvi, ufugaji wa samaki mwani na vitu vyengine vilivyokuwamo katika sekta hiyo.

"Kupata wataalamu sita naamini kwamba tunaweza kuzalisha wajasiriamali wengi, kuongeza ajira na kipato cha wananchi kwa kuamini kwamba pia pato la taifa litakua kutoka asilimia 4.4 na kwenda asilimia sita mpaka 7," alisema.

Aliipongeza kampuni hiyo kwa kukubali kufanya kazi na wizara katika sekta hiyo ya uchumi wa buluu kwa kuunganisha nguvu za kisheria.

Naye Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO), Ameir Haidar Mshenga, akitoa maelezo yaliyosababisha kuingia katika ushirikiano huo, alisema hivi sasa nchi kupitia serikali inatekeleza sera ya uchumi wa buluu na uvuvi.

Alisema wamekuwa wakipokea maagizo kutoka kwa Rais kuhakikisha wanakuza uchumi kupitia uchumi huo na kampuni ya ZAFICO imetafuta wawekezaji wengi ili kuhakikisha wanaingia nao ubia.

"Tumefanya mjadala na wawekezaji wengi, lakini kampuni hii ndio iliyosimama na kuonyesha nia ya kushirikiana na sisi katika kukuza sekta hii ya uchumi wa buluu," alisema.

Akiyataja maeneo ambayo watashirikiana na kampuni hiyo alisema ni pamoja na ujenzi wa kiwanda cha kutengenezea maboti kitakachojengwa katika eneo la Fungurefu Mkokotoni Mkoa wa Kaskazini Unguja, ambacho kitatengeneza boti kuanzia mita tano hadi za mita 30.

Mradi mwingine unaotarajiwa kutekelezwa kupitia ushirikiano huo ni wa kuchakata minofu ya samaki, dagaa, kutengeneza chakula cha samaki na mradi wa uvuvi wa bahari kuu, kutengeneza vyumba vya baridi na kiwanda cha kuzalisha barafu ambapo miradi hiyo itakamilika ndani ya miezi sita.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni hiyo, Zainulabdeen Mohamed Hairu, alisema kampuni yao ina uwezo mkubwa katika masuala ya uchumi wa buluu na kuahidi kushirikiana pamoja kuona dhana hiyo inafikiwa kwa vitendo.

Aliipongeza serikali kwa kuwaamini kuwapatia miradi hiyo na kuahidi kushirikiana katika kuona miradi hiyo inakamilika kwa kipindi walichokubaliana katika mkataba wao.

# MATANGAZO MCHANGANYIMO

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **KILOJA JOVINI DEOGRATIAS** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya PREMIO lenye namba za usajili **T566DGJ.**
Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/165841/2022.**
Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi au apige simu namba **0787956905.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **ERICK BINAMUNGU KAJUNA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari aina ya Fuso lenye namba za usajili **T570AXE**, chassis namba **FK618K501649.**
Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/168782/2022.**
Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi au apige simu namba **0764616937.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI KWA MDAIWA**
**MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU**
**WILAYA YA GEITA**
**SHAURI LA MADAI NA: 19/2022**
**MDAI: REBECA D/O ELIAS**
**DHIDI YA**
**MDAIWA: MASHAKA S/O JACKSON**
**WA BARA & VISIWANI**

**AMRI:-** Unaamriwa na Mahakama uhudhurie hapa Mahakamani mnamo tarehe 12/05/2022 saa 2:30 asubuhi bila kukosa. Usipohudhuria shauri hili laweza kusikilizwa upande mmoja bila ya wewe kuwepo na kutolewa uamuzi.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama leo ALHAMISI tarehe 21/04/2022.

MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA GEITA
HAKIMU
RESIDENT MAGISTRATE
GEITA.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HENRY MARIO MSIGWA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya MITSUBISHI FUSO yenye usajili namba T 571 ATW , CHASSIS NAMBA FM62FSZ750028. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**POLISI TAARIFA: SO/RB/235/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**OPTATUS ROMWALD MBILINYI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya JIEFANG yenye usajili namba **T 890 AMU ,** CHASSIS NAMBA **94071730.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
POLISI TAARIFA: **SO/RB/1607/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EDWARD WILSON NTILAKIGWA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA HIACE yenye usajili namba T 423 BUA , CHASSIS NAMBA LH1231014406. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**POLISI TAARIFA: SO/RB/1179/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**THOMAS VILGINI MBILINYI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya SANLG SL125 yenye usajili namba MC 966 AKW , CHASSIS NAMBA LBRSP-JB5989027509.
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**POLISI TAARIFA: SO/RB/3615/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**MAHAKAMA YA WILAYA DODOMA**
**RUFAA/MADAI/JINAI NA 23/2022**
**Shauri la Rufaa Jinai/Madai Na. 253/2022**
**Katika Mahakama ya WILAYA YA DODOMA**
**GEOFREY IBRAHIMU..................MRUFANI**
**DHIDI YA**
**DENIS ZANAKI........................MRUFANIWA**

**Kwa: DENIS ZANAKI**
Kwa rufaa iliyotajwa hapo juu itasikilizwa katika Mahakama iliyotajwa hapo juu siku ya 05 Mwezi 05 Mwaka 2022 unatakiwa uhudhurie katika Mahakama hiyo Mrufani/Mrufaniwa/Shahidi pamoja na vielelezo vyovyote kama vipo.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na mhuri wa Mahakama hii leo

Tarehe 06 Mwezi 04 Mwaka 2022

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
DODOMA
RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA DISTRICT

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT REGISTRY OF BUKOBA AT BUKOBA**
**MISC CIVIL APPLICATION No. 11/2022**
**(Originating from HC Civil case No. 1A of 2013 and Original HC Civil case No. 4 of)**
**ATHANAS SIMON .............................................APPLICANT**
**VERSUS**
**KABANGA NICKEL COMPANY LIMITED ........RESPONDENTS**

**TO;**
**KABANGA NICKEL COMPANY LIMITED**
**NGARA DISTRICT**
**KAGERA REGION**

**RE NOTICE FOR DATE OF HEARING**

Whereas the above mentioned Applicant has lodged a case registered as Misc Civil Application No. 11 of 2021 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.

Take notice that the above said case has been scheduled for hearing on 6th day of June, 2022 at 08:30 am before Hon. Ntemi, J. You are authorized to appear in person or through your Advocate. Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said hearing the case will proceed in your absence.

Given under my hand and seal of the court this **25th day of April, 2022.**

A.W.KABUKA
DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
BUKOBA

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



Martha Karua (kushoto) kutoka Chama cha Narc, ambaye ameteuliwa kuwa mgombea mwenza wa Raila Odinga, baada ya Azimio la Umoja - One Kenya kumpitisha, jana. Kiongozi wa chama cha Wiper, Kalonzo Musyoka (kulia). **PICHA: MTANDAO**

# Martha Karua rasmi mgombea mwenza wa Raila Odinga

**Nairobi,** KENYA

WAGOMBEA urais wa muungano wa Azimio la Umoja-OneKenya Alliance, Raila Odinga na Rais Uhuru Kenyatta, wamekubaliana kumteua Kiongozi wa Narc Kenya, Martha Karua kuwa mwaniaji mwenza katika muungano huo.

Awali Odinga alikuwa akimtaka mbunge wa zamani wa Gatanga, Peter Kenneth naye Rais Kenyatta alipendelea Waziri wa Kilimo Peter Munya, akasema mwandani wa Odinga aliyeomba jina lake libanwe kwa kuhofia kusutwa na vigogo wa Azimio.

Duru zilieleza kwamba katika mkutano uliofanyika Ikulu wiki iliyopita, Odinga aliambiwa kuchagua kati ya Musyoka na Karua kuwa mgombea mwenza wake.

"Odinga alimteua Karua na kusisitiza kuwa ikiwa ni lazima achukue mgombea mwenza kutoka eneo la Ukambani," alisema mwandani wa kinara wa ODM, Odinga.

Ilielezwa kuwa kauli hiyo ya Odinga ndiyo imekuwa ikimsukuma Musyoka kumshinikiza kubadilisha uamuzi wake na kumteua yeye.

Alipokuwa akizungumza mjini Kitui, juzi, Musyoka alisema kuwa muungano wa Azimio utapoteza urais iwapo Odinga hatamteua yeye kuwa mgombea mwenza wake.

**Munya ni mwanasiasa jasiri na mwenye msimamo mkali na huenda Odinga hataki naibu ambaye atampeleka mbio. Lakini Munya anaweza kumletea Odinga kura nyingi katika eneo la Mlima Kenya, haswa Meru.**

Imebainika kuwa wandani wa Rais Kenyatta, haswa kutoka eneo la Mlima Kenya wanaunga mkono Karua ambaye wanaamini atatetea masilahi yao vyema akiwa naibu wa rais, kutokana na msimamo wake mkali.

Pia wanaamini kuwa Karua atasaidia kuvutia kura nyingi za wanawake katika kikapu cha Odinga.

Mshauri wa Rais kuhusu masuala ya kisiasa, Prof. Mutahi Ngunyi pamoja na wanablogu wa Jubilee wamekuwa wakimpigia debe Karua katika mitandao ya kijamii.

Katikati mwa Aprili, kundi la viongozi wanawake walio ndani ya Azimio wakiongozwa na Ngilu walishinikiza kuteuliwa kwa Karua.

Kulingana na duru, kamati iliyoteuliwa kushauri kuhusu mwaniaji mwenza ilikuwa ni njia ya kupitisha chaguo la Rais Kenyatta na Odinga, na pia kutafuta njia ya kumtuliza Musyoka.

Miongoni mwa mbinu hizo ni kubuniwa kwa wadhifa wa mkuu wa mawaziri ambao atatengewa.

### KENNETH NA MUNYA

Juzi, kamati ya kuteua mgombea mwenza wa Azimio ilisema itakutana na wanaokimezea mate kiti hicho kati ya Mei 4 na Mei 20 ili wapigwe msasa kutambua anayefaa zaidi.

Hatua ya kambi ya Rais Kenyatta kutomtaka Kenneth, duru zinaeleza, inatokana na hofu kuwa huenda mbunge huyo wa zamani wa Gatanga akageuka kuwa mtu wa kufuata maagizo ya Odinga kwa urahisi, na hivyo kushindwa kutetea masilahi yao serikalini iwapo muungano wa Azimio utashinda Uchaguzi Mkuu wa Agosti 9, mwaka huu.

Rais Kenyatta, ilielezwa awali kuwa alikuwa akimpendelea Munya kwa imani kuwa ni kiongozi mwenye msimamo na aliye na uwezo wa kupigania masilahi ya eneo la Mlima Kenya bila woga.

Vilevile, wandani wa rais waliamini kuwa Munya anaweza kuleta sehemu kubwa ya zaidi kura 900,000 za eneo la Meru upande wa Odinga.

Profesa Macharia Munene, ambaye ni mhadhiri wa historia na mahusiano ya kimataifa, anakiri kuwa kuteuliwa kwa Munya kuwa mgombea mwenza wa Odinga kungeleta kura nyingi za urais katika kikapu cha Azimio.

"Munya ni mwanasiasa jasiri na mwenye msimamo mkali na huenda Odinga hataki naibu ambaye atampeleka mbio. Lakini Munya anaweza kumletea Odinga kura nyingi katika eneo la Mlima Kenya, haswa Meru," anasema Prof. Munene. **TAIFA LEO**

# EU yajadili kuondokana na kuitegemea nishati Russia

**Brussels,** UBELGIJI

MAZUNGUMZO kuhusu Umoja wa Ulaya (EU), unaweza kujiondoa kutoka kwa usambazaji wa nishati ya Russia, yamekuwa yakifanyika Brussels.

Waziri wa Uchumi Ujerumani, Robert Habeck (pichani), alisema nchi wanachama bado zimegawanyika juu ya vikwazo vya nishati ya Russia.

Hungary imeweka wazi upinzani wake wa kupiga marufuku mafuta na gesi ya Russia.



"Ujerumani yenyewe haiko tayari kupiga marufuku gesi ingawa itaweza kukabiliana na marufuku ya mafuta ya Russia kufikia mwisho wa mwaka," Habeck alisema.

Huo ndio wakati muafaka wa kuondolewa kwa mafuta yoyote ya Russia ambayo inaonekana kujadiliwa na nchi wanachama wa EU.

"Tumefaulu kufikia hali ambapo Ujerumani inaweza kubeba vikwazo vya mafuta," Habeck aliuambia mkutano wa wanahabari, ila alionya hii haimaanishi kuwa hakutakuwa na matokeo.

Ujerumani imepunguza sehemu ya Russia ya uagizaji wa mafuta kutoka asilimia 35 hadi 25, bado inafanya kazi kutafuta wasambazaji mbadala ambao wanaweza kuziba pengo ikiwa kutakuwa na marufuku kamili. **BBC**

# EU yasibiri kauli ya Modi mgogoro wa Russia, Ukraine

**New Delhi,** INDIA

WAZIRI Mkuu wa India, Narendra Modi, ameanza ziara yake barani Ulaya kwa kuzitembelea Ujerumani, Denmark na Ufaransa huku uamuzi wa serikali yake wa kukataa kulaani uvamizi wa Russia nchini Ukraine, unatarajiwa kuwa ajenda muhimu ya majadiliano.

Akizungumza kabla ya kupanda ndege mjini New Delhi, Modi amesema analenga kutumia ziara yake kuimarisha ari ya ushirikiano na mataifa ya Ulaya katika wakati kanda hiyo inakabiliwa na changamoto nyingi.

Modi amepangiwa kuwa na mazungumzo na Kansela Olaf Scholz wa Ujerumani mjini Berlin, kabla ya kuelekea Copenhagen ambako atajiunga na viongozi wa mataifa ya Scandinavia kwa mkutano wa siku mbili kati ya India na mataifa ya kanda hiyo.

Kadhalika atakwenda mjini Paris kwa ajili ya mkutano na Rais Emmanuel Macron kujadili masuala kadhaa ya dunia pamoja na ushirikiano kati ya India na Ufaransa. **DW**



# TFF YAZISHUSHIA RUNGU LA FAINI SIMBA, YANGA

**Na Adam Fungamwangwo**

KLABU za Simba na Yanga zimepigwa faini ya shilingi milioni nne kwa makosa mbalimbali yaliyojitokeza kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, huku Mbeya Kwanza ikitwangwa faini ya shilingi laki tano.

**Katika adhabu hizo, Yanga inaongoza kwa kutozwa faini kubwa, ambapo imepigwa faini ya shilingi milioni tatu, Simba ikikamuliwa shilingi milioni moja.**

Taarifa iliyotolewa jana na Bodi ya Ligi ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), imesema kuwa adhabu hizo zimetolewa baada ya kikao cha Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB), kilichokaa Aprili 27, mwaka huu kupitia mwenendo na matukio mbalimbali ya Ligi Kuu na kufanya maamuzi hayo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo ni kwamba klabu ya Yanga imetozwa faini ya shilingi milioni mbili kwa kosa la kuingia kwenye mlango usio rasmi katika mechi yao dhidi ya Azam FC iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, Aprili 6, mwaka huu na kushinda mabao 2-1.

Adhabu hiyo ni kwa mujibu wa kanuni ya 27: (21 & 60) ya Ligi Kuu kuhusu taratibu za michezo.


Klabu ya Yanga, pia imetozwa faini ya shilingi milioni moja kwa kosa la mashabiki wake kumrushia chupa mwamuzi msaidizi wa mchezo huo namba 151 dhidi ya Azam, na hii ni kwa mujibu wa kanuni ya 47:1 ya Ligi Kuu Udhibiti wa Klabu.

Kwa upande wa Klabu ya Simba, nayo imetozwa faini ya shilingi milioni moja kwa kosa la mashabiki wake kurusha chupa uwanjani baada ya mchezaji Meddie Kagere kufunga bao la pili dakika za mwisho za mchezo uliocheza Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, Aprili 7, mwaka huu. Adhabu hiyo ni kwa mujibu wa kanuni ya 47:1 ya Ligi Kuu kuhusu udhibiti.

Klabu ya Mbeya Kwanza imepewa onyo na kutozwa faini ya shilingi laki tano kwa kosa la mashabiki wake na baadhi ya viongozi kuvamia uwanja, kushambulia pamoja na wachezaji baada ya kumalizika kwa mechi kati ya Mbeya Kwanza, Uwanja wa Majimaji mjini Songea, Aprili 23, mwaka huu.

Hii ni mara ya kwanza kwa timu hiyo kufanya kosa hilo. Adhabu hiyo ni kwa mujibu wa kanuni ya 47:1 ya Ligi Kuu Udhibiti kwa Klabu.

**UMETISHA...**




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), ambayo ni Mdhamini Mkuu wa Ligi Kuu ya Soka Tanzania Bara (NBC Premier League), Theobald Sabi (kushoto), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya shilingi milioni moja kwa mchezaji wa Klabu ya Simba, Clatous Chama, aliyetangazwa mchezaji bora wa ligi hiyo kwa mwezi Machi wakati wa mechi kati ya Simba na Yanga iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumamosi iliyopita. Timu hizo zilitoka sare ya bila kufungana. Anayeshuhudia ni Meneja Uhusiano wa benki hiyo, Godwin Semunyu. **MPIGAPICHA WETU**

## BFT sasa yaja na Kilimanjaro Mountain

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Ngumi za Ridhaa Tanzania (BFT), limeandaa mashindano ya kirafiki ya kimataifa yaliyopewa jina 'Kilimanjaro Mountain', ambayo yamepangwa kufanyika Mei 27 hadi 31, mwaka huu kwenye Uwanja wa Ndani wa Taifa, Dar es Salaam.

Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zinajiandaa kupeleka wachezaji wa michezo mbalimbali ikiwamo mchezo wa ngumi kushiriki mashindano ya Jumuiya ya Madola yatakayofanyika Julai mwaka huu nchini Uingereza.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Katibu Mkuu wa BFT, Abubakari Mohammed, alisema lengo ni kuwapima nguvu mabondia ili kutoa fursa ya kuangalia kasoro zifanyiwe maboresho kabla ya kuelekea katika mashindano ya kimataifa.

Alisema nchi ambazo tayari zimethibitisha kushiriki ni Sudan Kusini, Botswana, Msumbiji, Burundi, Zambia, Malawi, Uganda, DRC Congo, Zimbabwe na wenyeji Tanzania, ambao watawakilishwa na Klabu ya Magereza, JKT na Ngome.

"Mashindano haya ni kwa ajili ya kuwapima nguvu mabondia na tuna imani kuwa nchi tulizozialika asilimia kubwa zinashiriki na Jumuiya ya Madola, itakuwa kipimo kizuri, na kuwapa changamoto," alisema Mohammed.

Alisema maandalizi yanaendelea vizuri na tayari serikali imebeba jukumu la kugharamia malazi, chakula na usafiri wa ndani kwa timu zitakazoshiriki mashindano hayo.

Mashindano hayo yatashirikisha mabondia wanawake, lengo likiwa ni kuwapa uzoefu wa kushiriki kwa manufaa michuano ya kimataifa.

# Tanzania Prisons yaapa kutoshuka daraja

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwangwo**

WAKATI Kocha Mkuu wa Tanzania Prisons, Patrick Odhiambo, akisema kuanzia sasa anataka kukusanya pointi 3 katika kila mchezo wa Ligi Kuu Bara uliopo mbele yao, nahodha wa timu hiyo, Jumanne El Fadhili, amesema wanaodhani watashuka daraja, basi watasubiri sana.

Kauli hiyo ilikuja baada ya juzi kuipa kichapo cha bao 1-0 timu ya Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, hivyo kupanda kutoka nafasi ya 15 hadi ya 13, ikiwa na pointi 22 huku Polisi Tanzania ikibaki kwenye nafasi ile ile ya nane na alama zake 25.

Akizungumza na gazeti hili jana, kocha huyo alisema licha ligi kuwa ngumu atahakikisha hawashuki daraja.

"Mchezo ulikuwa na ushindani isipokuwa tunashukuru tumepata pointi tatu," alisema Odhiambo.

Kwa upande wa nahodha wa timu hiyo, El Fadhili, ambaye alipachika bao hilo pekee kwenye mechi hiyo, alisema kwa sasa wapo vizuri tofauti na mwanzo na wana uhakika wa asilimia nyingi za kubaki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

El Fadhili alisema kilichosababisha kupoteza michezo mingi hasa kwenye raundi ya kwanza ni wachezaji wengi kuathirika kisaikolojia, lakini kwa sasa baada ya kupata ushindi mfululizo, wamekuwa na morali na mechi za hivi karibuni wameonekana kupambana kusaka matokeo.

"Unajua unapofungwa, ukienda kwenye mechi nyingine unakuwa na wasiwasi na hujiamini, hivyo ukifanya masihara unaweza kupoteza. Hicho ndicho kilichokuwa kinatukumba sisi Prisons, unajua tuna baadhi ya wachezaji chipukizi kwa hiyo hawajazoea hali hiyo," alisema kiungo huyo mkabaji.

Alikiri kuwa ni kweli mpaka sasa hawapo kwenye hali nzuri, lakini ana uhakika kuwa timu yao itabaki Ligi Kuu.

"Hilo wala halina wasiwasi, tutabaki Ligi Kuu kwa sababu kwa sasa tupo vizuri sana. Ni kweli Prisons hatujawa vile ambavyo Prisons inavyokuwa miaka yote, lakini hapa tulipo sasa hakuna wa kutuzuia, tunabaki Ligi Kuu," alisema.

Naye Mohamed Mmanga, mchezaji wa Polisi Tanzania alisema wameumia sana kufungwa na Prisons.

"Tumeumia sana na inauma sana kufungwa na kutopata ushindi kwenye mechi za karibuni, lakini ndiyo mpira kwa sababu wao walipambana zaidi kwa sababu wako kwenye hali mbaya," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RASHFORD HAKIELEWEKI UNITED

MSHAMBULIAJI wa England, Marcus Rashford, 24, amehusishwa na habari za kuondoka katika klabu ya Manchester United, lakini atapewa fursa ya kuthibitisha iwapo anapaswa kusalia katika klabu hiyo chini ya kocha mpya, Erik ten Hag. ***(Sun)***

### MAGALHAES KUTUA JUVE

MLINZI wa Arsenal na raia wa Brazil, Gabriel Magalhaes mwenye umri wa miaka 24, huenda akahamia katika klabu ya Juventus mwishoni mwa msimu huu. ***(Gianluca Di Marzio, via Teamtalk)***

### LEWANDOWSKI BADO MADRID

MKURUGENZI wa Klabu ya Barcelona, Mateu Alemany amekana kwamba klabu hiyo ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, imekutana na wakala wa mshambuliaji wa Bayern Munich, Robert Lewandoowski kuhusu uhamisho wa mchezaji huyo mwishoni mwa msimu huu. ***(Movistar, via Goal)***

### RICE AGOMBEWA ENGLAND

KIUNGO wa kati wa West Ham, Declan Rice, amehusishwa na klabu za Chelsea, Manchester City na Manchester United. ***(Sky Sports News)***

### NEVES AWINDWA OLD TRAFFORD

MANCHESTER United ilimtuma skauti wake kumtazama kiungo wa kati wa Ureno, Ruben Neves akiichezea Wolves katika mechi ambayo klabu hiyo ilifungwa na Brighton 3-0 Jumamosi. Klabu hiyo ya Old Trafford imedaiwa kuwa na nia ya kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Birmingham Live)***

### JORGINHO AMULIKWA JUVE

JUVENTUS inataka kumsajili kiungo wa kati wa Chelsea, Jorginho kurudi katika klabu hiyo ya Ligi ya Serie A, huku mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, ukitarajiwa kumalizika 2023. ***(Todofichajes)***

### ALONSO KURUDI HISPANIA

MLINZI wa kushoto wa Chelsea, Marcos Alonso ni mmoja wa wachezaji ambao klabu ya Barcelona inataka kuwasajili, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, akitaka kurudi nchini Hispania mwishoni mwa msimu huu. ***(Fabrizio Romano, via Marca)***

### TIELEMANS AITAKA MADRID

KIUNGO wa kati wa Ubelgiji, Youri Tielemans ambaye ana mkataba na klabu ya Leicester City hadi 2023, angependelea uhamisho wa kuelekea Hispania iwapo ataondoka katika klabu hiyo. Real Madrid wanaaminika kuwa na nia ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Sacha Tavolieri, via Mail)***


### BROJA AWANIWA NAPOLI

NAPOLI ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Chelsea, Armando Broja, 20, huku mshambuliaji huyo wa Albania akionyesha mchezo mzuri wakati huu akicheza kwa mkopo katika Klabu ya Southampton msimu huu. ***(Todofichajes)***

### LINGARD KUBAKI MAN U

KIUNGO wa kati wa England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 29, huenda akasalia katika klabu hiyo. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TUCHEL ATAJA SABABU KUTOMCHEZESHA LUKAKU

Alipoulizwa na waandishi wa habari baada ya mchezo huo kuhusu kutomchezesha, alijibu...

**LONDON,** England

THOMAS Tuchel amejaribu kueleza ni kwa nini Romelu Lukaku alibaki benchi na kutotumika wakati Chelsea ilipochapwa bao 1-0 na Everton kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, Jumapili.

Bao lililowekwa kimiani na Richarlison baada ya Azpilicueta kufanya kosa liliigharimu timu, lakini maswali zaidi yakiulizwa kuhusu uwepo wa mshambuliaji huyo wa Ubelgiji hapo Stamford Bridge.

Chelsea walisafiri mpaka Goodison Park kuchuana na Everton ambao wanapambana kuepuka kushuka daraja wakati huo huo 'The Blues' walikuwa wakitafuta kujikita kwenye nne bora.

**Tuchel aliamua kutomwanzisha mshambuliaji Lukaku wakati kikosi chake kilipohitaji msukumo wa kushambulia kipindi cha pili.**

Lakini aliamua kuwaingiza Christian Pulisic na Hakim Ziyech wakati akisaka bao la kusawazisha.

Alipoulizwa na waandishi wa habari baada ya mchezo huo kuhusu kutomchezesha Lukaku, Tuchel alijibu: "Kwa sababu tulimtoa Jorginho. Tulikuwa na mabadiliko matatu tu."

Chelsea, ambayo imeshuhudia Lukaku akishindwa kufunga bao la Ligi Kuu tangu Desemba 29, mwaka jana, itarejea uwanjani wikendi ijayo itakapocheza na Wolves.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,224

MECHI KALI
NAMUNGO
VERSUS
SIMBA
1 | 5.45
X | 3.31
2 | 1.63

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ARTETA APIGIA HESABU KUMALIZA YA TATU EPL



**LONDON,** England

MIKEL Arteta ana matumaini ya kuipiku Chelsea nafasi ya tatu, ingawa anatarajia kwamba nafasi ya Arsenal ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya itatimia baada ya ushindi "mbaya" dhidi ya West Ham.

Arsenal walicheza mechi ya Jumapili usiku baada ya Chelsea iliyo nafasi ya tatu na Tottenham iliyo nafasi ya tano kucheza mapema siku hiyo.


Chelsea walifungwa na Everton, lakini Spurs waliwafunga Leicester City na kuwatangulia kwa muda wapinzani wao katika nafasi nne za juu.

Arsenal walikuja na jibu muhimu, kwa kuwalaza West Ham 2-1 kwenye Uwanja wa London na kurudi nafasi ya nne na wamepitwa alama tatu na Chelsea, huku Thomas Tuchel akikiri wasiwasi wake kuhusu matumaini ya timu yake kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kocha Arteta hakufurahishwa na uchezaji wa 'Washikabunduki hao, lakini alitambua umuhimu wa ushindi huo.

"Hatukuruhusu mabao, lakini hatukucheza vizuri," alisema akiiambia Sky Sports. "Ikibidi nichambue mchezo, ningetumia neno ambalo ni ushindi mbaya, leo (juzi) tumeshinda, lakini ushindi mbaya.

"Timu kubwa zinapaswa kutafuta njia ya kushinda wakati hazicheza kwa ubora wao, na leo (juzi) tulishinda, lakini hatukucheza vizuri sana."



## Xavi: Barca ina nafasi Uef

**BARCELONA,** Hispania

XAVI amesema ushindi wa mabao 2-1 wa Barcelona dhidi ya Real Mallorca umewapa "amani ya akili" katika harakati zao za kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, na akampongeza Memphis Depay baada ya kufunga bao.

Wakiwa wamepoteza mechi tatu mfululizo kwenye Uwanja wa Camp Nou kwa mara ya pili tu katika historia yao na 'Blaugrana' hao waliibuka tena kupitia mabao bora kutoka kwa Depay na Sergio Busquets, wakishikilia ushindi huo baada ya Antonio Raillo kurudisha bao dakika za mwisho.

Miamba hiyo ya Katalunya sasa imeshinda mechi tano kati ya saba zilizopita kwenye LaLiga na hivyo kuwazidi pointi tisa Real Betis walio katika nafasi ya tano katika kinyang'anyiro cha kuwania kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, na sasa wapo nafasi ya pili.

Ingawa Xavi alisisitiza kwamba timu yake ilipaswa kushinda mechi hiyo kwa raha zaidi, alifurahishwa na kupata ushindi muhimu katika harakati zao za kumaliza kwenye nne bora.

"Ilikuwa mechi ya kushinda 3-0 na tu-
napaswa kuridhika
di, tungefanya zaidi.
mchezo wa kushin
alisema Xavi baada
ushindi huo.

Bao la kwanza la
pay kwa shuti kali li
fanya kufikisha ma
11 msimu huu kwe
LaLiga - akiwa a
funga mengi zaidi
mchezaji yeyote wa
celona.

Na Xavi hakuwa ta
kujadili kama msh
buliaji huyo ana m
takabali hapo Ca
Nou, kwani alisisi
nyota huyo mwe
umri wa miaka 28,
tahili kucheza baad
kuonyesha kiwango
zuri kwenye mazoez

## HABARI MICHEZO

# SERENGETI GIRLS YAKARIBIA KOMBE LA DUNIA INDIA 2022

Na Adam Fungamwango

TIMU ya Taifa ya Wasichana chini ya miaka 17, Serengeti Girls, imesonga mbele kwenye mechi ya mchujo kuwania tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Dunia chini ya umri huo, linalotarajiwa kufanyika baadaye mwaka huu nchini India, baada ya kuiondosha mashindanoni Burundi kwa jumla ya mabao 5-2.

Licha ya juzi usiku kufungwa mabao 2-1 na timu ya Taifa ya Burundi, Tanzania inasonga mbele kutokana na ushindi wa mabao 4-0 iliyoupata mwezi uliopita nchini Burundi.

Kwa matokeo hayo, timu hiyo sasa itamenyana na timu ya Taifa ya Cameroon kwenye mechi ya mwisho ya mchujo, kabla ya kufuzu kwenye fainali hizo.

**Cameroon imepata nafasi ya kucheza na Serengati Girls, baada ya kuiondoa kwenye mashindano Zambia.**

Fainali hizo za Kombe la Dunia zitaanza kutimua vumbi nchini India kuanzia Oktoba 11 hadi 30, mwaka huu.

Wakati huo huo, mchezaji wa Kitanzania, Clara Luvanda anaongoza katika orodha ya wafungaji kwenye mechi za kutafuta tiketi ya kufuzu Kombe la Dunia chini ya miaka 17.

Luvanda, anayeichezea klabu ya Yanga Princess, anaongoza akiwa na mabao saba, huku wanaomfuatia ambao ni Yasmine Zouhir wa Morocco na Opeyemi Ajakale wa Nigeria wakiwa na mabao matano kila moja.

Mtanzania mwingine Aisha Juma anaiongoza safu ya wachezaji waliofunga mabao matatu mpaka sasa.

Aisha anayeichezea Simba Queens ana mabao hayo akifuatiwa na Camila Daha wa Cameroon, Georgina Aoyem wa Ghana, Doha El Madani wa Morocco na Omowunmi Bello wa Nigeria.



# GEITA GOLD YAOTA KUCHEZA KIMATAIFA

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Geita Gold imeonyesha kuridhishwa na mwenendo wake wa Ligi Kuu msimu wa kwanza tu tangu kupanda, ikisema malengo yake kwa sasa ni kupata nafasi za juu ambazo zinaweza kuiwezesha kucheza mechi za kimataifa msimu ujao.

Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Simon Shija amesema ni maendeleo makubwa walioyapata msimu wao wa kwanza tu tangu kupanda, lakini wameitengeneza timu ambayo imekuwa ya kuhofiwa sana msimu huu.

"Tumetengeneza timu imara, hasa mzunguko wa pili, tumeridhishwa kabisa na mwenendo wetu msimu huu, hasa ikizingatiwa ndiyo kwanza tumepanda, tumekuwa timu tishio kwenye Ligi Kuu, na tunaendelea kuwa hivyo hadi mwishoni mwa ligi. Lengo letu ni kusalia kwenye nafasi za juu, lakini ikiwezekana kupata nafasi moja ya juu ambayo inaweza kufanya tukacheza mechi za kimataifa msimu ujao," alisema Shija.

Geita Gold inashika nafasi ya sita kwenye Ligi Kuu ikiwa na pointi 28. Timu hiyo ilianza ligi kwa kusuasua, lakini ikawa ndiyo timu pekee ambayo ilitumia vizuri zaidi dirisha dogo la usajili kwa kufanya usajili wa wachezaji wengi wenye viwango vya hali ya juu na wazoefu kama kina Kelvin Yondani, Juma Nyosso, Lucian William 'Gallas', na wengine wengi ambao wameshawahi kuzichezea klabu kubwa za Simba na Yanga.

Msimu huu, timu itakayoshika nafasi ya tatu, itacheza Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao, kwani Tanzania itapeleka jumla ya timu nne, ambao ni washindi wawili wa juu kwenye Ligi Kuu watacheza Ligi ya Mabingwa Afrika, wa tatu na bingwa wa Kombe la FA, watakwenda kucheza Kombe la Shirikisho.


# 4,601,040 JACKPOT

## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 07/05/22 | 17:00 | Burnley vs Aston Villa | 2.87 | 3.17 | 2.41 |
| 02. 07/05/22 | 17:00 | Brentford vs Southampton | 2.21 | 3.37 | 3.02 |
| 03. 07/05/22 | 19:00 | Sassuolo vs Udinese | 2.25 | 3.56 | 2.82 |
| 04. 07/05/22 | 19:30 | Brighton vs Manchester Utd | 2.62 | 3.21 | 2.58 |
| 05. 07/05/22 | 19:30 | Hertha BSC vs Mainz | 2.52 | 3.31 | 2.62 |
| 06. 07/05/22 | 20:00 | Benfica vs Porto | 2.74 | 3.43 | 2.39 |
| 07. 08/05/22 | 16:00 | Leicester vs Everton | 2.31 | 3.22 | 2.97 |
| 08. 08/05/22 | 16:00 | Venezia vs Bologna | 2.93 | 3.27 | 2.31 |
| 09. 08/05/22 | 17:15 | Villarreal vs Sevilla FC | 2.30 | 3.25 | 3.05 |
| 10. 08/05/22 | 17:45 | Feyenoord vs PSV Eindhoven | 2.41 | 3.62 | 2.58 |
| 11. 08/05/22 | 19:00 | Salernitana vs Cagliari | 2.35 | 3.26 | 2.87 |
| 12. 08/05/22 | 19:30 | Espanyol vs Osasuna | 2.59 | 3.14 | 2.74 |
| 13. 08/05/22 | 22:00 | Atletico Madrid vs Real Madrid | 2.37 | 3.30 | 2.90 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 03/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 2469 | Chungnam Asan vs Anyang | 2.63 | 3.07 | 2.53 |
| 14:00 | 2281 | Perth SC vs Floreat Athena | 2.04 | 3.99 | 2.77 |
| 14:30 | 2378 | Churchill Brothers vs Minerva FC | 2.76 | 3.30 | 2.30 |
| 15:00 | 3039 | Ipswich U23 vs Sheffield United U23 | 2.63 | 3.99 | 2.13 |
| 15:00 | 4092 | Alashkert Martuni vs Urartu | 2.36 | 2.85 | 3.35 |
| 15:00 | 5886 | Cardiff City U23 vs Crewe U23 | 1.46 | 4.58 | 5.07 |
| 15:00 | 5990 | Millwall U23 vs Sheffield Wednesday U23 | 2.16 | 3.55 | 2.82 |
| 15:30 | 2670 | QPR U23 vs Wigan U23 | 2.40 | 3.46 | 2.54 |
| 15:30 | 3340 | Keshla FK vs Sabayil | 1.59 | 3.55 | 5.25 |
| 16:00 | 1966 | Namungo vs Simba | 5.45 | 3.31 | 1.63 |
| 16:00 | 2303 | Watford U23 vs Barnsley U23 | 2.37 | 4.00 | 2.34 |
| 16:00 | 5522 | Kagera Sugar vs Azam | 2.93 | 2.69 | 2.59 |
| 16:05 | 4613 | Orgryte IS U21 vs Norrby IF | 2.53 | 3.89 | 2.24 |
| 16:30 | 2787 | Padideh Mashhad vs Sanat Naft Abadan | 3.69 | 2.47 | 2.36 |
| 17:00 | 5489 | IF Elfsborg U21 vs BK Hacken | 2.80 | 3.90 | 2.19 |
| 17:30 | 3540 | Gokulam Kerala FC vs Neroca FC | 1.48 | 4.18 | 5.44 |
| 17:30 | 5781 | Mezokovesdi SE vs Debreceni VSC | 1.95 | 3.46 | 3.36 |
| 17:45 | 3725 | Kukesi vs Partizani Tirana | 2.20 | 2.88 | 3.37 |
| 18:00 | 2001 | SuperSport Utd vs Stellenbosch | 2.25 | 2.73 | 3.72 |
| 18:00 | 2261 | FK Panevezys vs FC Hegelmann Litauen Kaunas | 2.70 | 3.10 | 2.65 |
| 18:00 | 2590 | Moroka Swallows FC vs Amazulu | 2.83 | 2.68 | 2.83 |
| 18:00 | 3726 | FK Zeljeznicar Banjaluka vs FK Alfa Modrica | 1.40 | 4.37 | 6.41 |
| 18:00 | 4527 | Karabakh vs Sabah | 1.28 | 4.87 | 8.97 |
| 18:00 | 5106 | Lietava Jonava vs Futbolo Akademija Siauliai | 13.66 | 6.63 | 1.14 |
| 18:00 | 5296 | Esperance Tunis vs US Monastir | 2.04 | 2.62 | 4.37 |
| 18:00 | 5421 | Inter Turku vs HJK Helsinki | 3.11 | 3.11 | 2.19 |
| 18:30 | 2530 | Ararat Armenia vs FC Noravank | 1.33 | 4.48 | 8.18 |
| 18:30 | 3179 | Sekhukhune United vs Mamelodi Sundowns | 5.60 | 3.35 | 1.68 |
| 18:30 | 4631 | MES Rafsanjan vs Fajr Sepasi | 1.71 | 3.01 | 5.44 |
| 19:00 | 2389 | LKS Lodz Pss vs Widzew Lodz | 2.29 | 3.07 | 2.97 |
| 19:00 | 2883 | FC Pipinsried vs Bayreuth | 6.22 | 4.56 | 1.39 |
| 19:00 | 4544 | Naft Masjed Soleyman FC vs Teraktor Sazi | 3.50 | 2.48 | 2.43 |
| 19:30 | 1540 | Videoton FC vs Budapest Honved | 1.95 | 3.45 | 3.35 |
| 19:30 | 3363 | TSV Rain/Lech vs Nurnberg II | 3.46 | 3.55 | 1.89 |
| 19:30 | 3734 | FC Juniors OO vs FC Liefering | 4.48 | 3.99 | 1.60 |
| 20:00 | 2420 | Illertissen vs SC Eltersdorf | 1.51 | 4.18 | 5.06 |
| 20:00 | 2502 | Seligenporten vs ASV Cham | 3.79 | 4.08 | 1.69 |
| 20:00 | 3044 | Buchbach vs Augsburg II | 2.44 | 3.37 | 2.54 |
| 20:00 | 5480 | 1. SC Feucht vs DJK Vilzing | 4.47 | 4.08 | 1.58 |
| 20:00 | 5829 | Halmstads BK vs Ostersunds | 1.45 | 4.23 | 7.45 |
| 20:30 | 3994 | Kaizer Chiefs vs Marumo Gallants FC | 1.78 | 3.20 | 5.00 |
| 21:00 | 1917 | Atsv 1898 Erlangen vs Eintracht Bamberg | 2.12 | 3.84 | 2.72 |
| 21:00 | 3566 | Bournemouth vs Nottingham | 2.19 | 3.21 | 3.21 |
| 21:05 | 4667 | Partick Thisle vs Inverness | 2.46 | 3.05 | 2.95 |
| 21:45 | 1602 | Edinburgh City vs Dumbarton | 2.81 | 3.35 | 2.32 |
| 21:45 | 1682 | Montrose vs Airdrieonians | 2.52 | 3.26 | 2.62 |
| 21:45 | 1902 | Chelmsford vs Concord Rangers | 2.20 | 3.40 | 3.10 |
| 21:45 | 3871 | Annan Athletic vs Forfar Athletic | 2.39 | 3.36 | 2.71 |
| 22:00 | 1157 | Real Santander vs Universitario Popayan | 1.63 | 3.55 | 4.86 |
| 22:00 | 1547 | Villarreal vs Liverpool | 4.37 | 3.92 | 1.68 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Mei 3, 2022

Nipashe




Ataja sababu kutomchezesha Lukaku

UKURASA 21

TUTAKIWASHA...



Wachezaji wa Simba baada ya kuwasili mkoani Lindi jana tayari kwa mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Namungo FC itakayopigwa kwenye Uwanja wa Ilulu leo. **PICHA: SIMBA**

## Yanga, Ruvu Shooting mechi ya pointi, rekodi

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema wameenda kupambana kutafuta pointi muhimu dhidi ya Ruvu Shooting katikka mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Yanga imewasili Kigoma tayari kuvaana dhidi ya wenyeji wao, Ruvu Shooting kwenye mchezo wa ligi hiyo utakaopigwa kesho, Jumatano katika dimba la Lake Tanganyika, mkoani humo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaze alisema baada ya Kariakoo 'Derby', walirejea mazoezi kufanyia kazi mapungufu yao ikiwamo kuongeza umakini kwa safu ya ushambuliaji katika umaliziaji wa nafasi wanazotengeneza.

Alisema wanahitaji kupambana kila mechi kutafuta pointi tatu ili kufikia malengo yao ya Yanga kutwaa taji la Ligi Kuu msimu huu, lakini kuweka rekodi ya kutopoteza mechi.

"Siwezi kusema kwamba hatutapoteza ila mipango yetu ni kuona tunapambana na ikiwezekana tunaweka rekodi ya kumaliza ligi bila ya kupoteza kwa sababu ligi imekuwa ngumu, kikubwa tujitume ili kutafuta matokeo mazuri katika michezo iliyopo mbele yetu," alisema Kaze.

Kwa upande wa Ofisa Habari wa Ruvu Shooting, Masau Bwire, alisema wanakwenda kuvunja mwiko wa Yanga.

"Hatuwezi kuwapelekea mechi mashabiki wa Kigoma, halafu tufungwe kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, naona Simba wameshindwa kuwafunga Yanga, sisi tunakwenda kutekeleza hilo kwa vitendo, hakuna mbwembwe nyingi, tutavunja mwiko wa kutofungwa na wale wanaotetema, wanatetemeka kwa mashaka," alisema Masau.

# Morrison safi Simba vs Namungo leo

## ●●● Inonga akunwa na nguvu ya mashabiki Mtwara wakipokelewa kifalme, awaahidi...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, baada ya kutoka suluhu dhidi ya watani wao wa jadi, Yanga, leo watakuwa kwenye Uwanja wa Ilulu mjini Lindi kucheza dhidi ya Namungo.

**Utakuwa ni mchezo wa 21 kwa upande wa Simba, huku Namungo ikicheza mechi 22, zikifuatana kwenye msimamo, mabingwa watetezi wakiwa na pointi 42, wenyeji wa mechi hiyo wakiwa na alama 29.**

Wakati Simba ikijaribu kuufukuzia ubingwa ambao unaonekana kabisa kuelekea kwa watani wa wa jadi, Yanga, Namungo itakuwa ikizitafuta pointi tatu kwa ajili ya kung'ang'ania kwenye nafasi ya tatu ili kupata tiketi ya kucheza mechi za kimataifa msimu ujao.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema kati ya wachezaji waliosafiri, yupo Bernard Morrison ambaye alishikiliwa na Jeshi la Polisi kwa saa chache Jumamosi baada ya mechi kati ya Yanga dhidi ya Simba kwa madai ya kumjeruhi shabiki.

"Tunakwenda kucheza mechi nyingine leo, pamoja na kwamba ratiba imebana sana. Jumamosi tumecheza na Yanga, siku hiyo hiyo tukaawapa ruhusa wachezaji wetu, kesho yake Jumapili wakarejea mazoezini, leo tupo kwenye mechi. Kiukweli imebana sana hata kocha wetu Pablo (Franco), amelalamikia hili, lakini hakuna namna ni lazima tupambane," alisema.

Alisema siku zote mechi dhidi yao na Namungo inakuwa na mvuto na ushindani mkubwa kutokana na wapinzani wao kuwa na wachezaji wazoefu kwenye ligi, baadhi wakiwa wamepita kwenye kikosi hicho.

Kuhusu sakata la Morrison amesema kuwa hawezi kusema lolote zaidi ya kuwaachia Jeshi la Polisi lifanye kazi yake, lakini alithibitisha kushikiliwa kwa saa kadhaa.

"Ni kweli Morrison alishikiliwa kwa saa kadhaa, lakini akaachiwa na akajiunga na wenzake kambini, na amesafiri na wenzake, yupo fiti kwa ajili ya mechi ya Namungu, suala hilo tumeliachia kwa Jeshi la Polisi, yaliyotokea si ndwele tugange yajayo, maisha yanaendelea kama kawaida," alisema Ahmed.

Hata hivyo, kwenye mechi hiyo, Simba itamkosa Saido Kanoute ambaye aliumia kwenye mechi dhidi ya Yanga ambaye alibaki Dar es Salaam kwa ajili ya matibabu.

"Tumekuja na wachezaji wote, kasoro Kanoute ambaye aliumia kwenye mechi ya Yanga, amebaki ili kupata vipimo ili kuangalia kwa kiasi gani aliumia, ili aanze matibabu. Baada ya kufanyika vipimo tutawaeleza."

Wakati huo huo, beki kisiki wa timu hiyo, Henoc Inonga 'Varane', amekunwa na namna mashabiki wa timu hiyo wanavyoonyesha mapenzi makubwa kwa timu yao kila wanapokwenda.

Inonga alitoa kauli hiyo baada ya kikosi cha Simba kuwasili Mtwara jana asubuhi na kupata mapokezi makubwa huku jina lake likiimbwa na mamia ya mashabiki waliojitokeza kuwalaki kutokana na kazi kubwa aliyoifanya ya kumdhibiti mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, kwenye mechi ya 'dabi' Jumamosi iliyopita ambayo ilimalizika kwa sare tasa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

'Mashabiki wetu wanaonyesha mapenzi makubwa kwetu, hii inatuongezea morali hata tukiwa uwanjani kujituma kuhakikisha tunawapa furaha. Bado hatujakata tamaa ya ubingwa, tutaendelea kupambana hadi mechi yetu ya mwisho, tunajua haitakuwa rahisi, lakini hakuna kinachoshindikana," alisema.

Naye Meneja wa Namungo, Steven Josiah, amesema kuwa kwa sasa kikosi chao kipo kwenye mazoezi makali kujiandaa na mechi hiyo, huku akitaraji kupata ushindi kwenye mechi hiyo wakitaka kulipiza kisasi baada ya kufungwa bao 1-0 kwenye mechi ya mzunguko kwa kwanza lililofungwa dakika za majeruhi na Meddie Kagere.

"Nguvu kubwa tunayoiweka kwa sasa ni kuhakikisha tunapata matokeo mazuri kwenye mechi zote zinazokuja, ikiwamo hii ya Simba, lengo letu turejee tena kwenye michuano ya kimataifa, alisema meneja huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >